

**WAKILI ZA SIMULIZI BUNILIZI KATIKA UTENDI WA
MIKIDADI NA MAYASA.**

NA

KIMANI PAULINE W.

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI
YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA
CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

University of NAIROBI Library



0389619 8

JULAI 2012

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote kile, kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.




22/10/2012

Kimani Pauline W.

Tarehe

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.



6/11/12

Profesa Kineene wa Mutiso

Tarehe

(Mtahini)



12TH NOV 2012

Daktari Rayya Timammy

Tarehe

(Mtahini)

TABARUKU

Naitabarukia kazi hii mwenda zake babangu Bw. Ibrahim Kimani na mwenda zake mamangu Bi. Lucy Wambui kwa kujinyima ili kunilea na kunielimisha na kunihakikishia msingi bora. Mungu awalaze mahali pema peponi. Aidha ninawatabarukia mume wangu mpendwa Bw. George Njoroge na mtoto wetu Peter Mungai kwa usaidizi wao wa kila aina, Mungu awajalie mema maishani.

SHUKRANI

Imekuwa safari ndefu mno tangu nilipoanza masomo haya. Safari yenyewe imekuwa na panda shuka nyingi sana lakini imefanikishwa na kufikia tamati kutokana na usaidizi wa watu wengi. Sina budi kuwatolea shukrani zangu za dhati japo sitaweza kuwataja wote.

Kwanza, ninamshukuru Mungu kwa kunijalia uwezo, siha na maarifa ya kukamilisha shahada hii ya uzamili.

Naishukuru familia yangu kwa kunihimiza kusoma, kunivumilia nikiwa masomoni na ufadhili wao wa kila aina. Namtolea shukrani za dhati mtoto wetu Peter Mungai aliyenisaidia sana katika kupiga chapa na kukaa nami usiku nikisoma. Alikuwepo wakati wowote nilipomhitaji.

Namkumbuka mwenda zake mama mkwe wangu Margaret Mungai aliyetuacha juzi tu kwa msukumo mkubwa wa maombi na kunipa moyo wa kuendelea na masomo yangu. Mungu amrehemu.

Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu, Dkt. Rayya Timammy na Prof. Kineene wa Mutiso kwa ushauri, mafunzo na maelekezo walionipa yaliyoniwezesha kukamilisha kazi hii.

Aidha, ninawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Isimu na Lugha katika Chuo Kikuu cha Nairobi kwa masomo na maarifa walionilimbikizia. Wahadhiri hawa ni pamoja na: Prof. Abdulaziz Mohammed, Prof. Habwe John, Prof. Kithaka wa Mberia,

Dkt. Mbatiah Mwenda, Dkt. Olali Tom, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Buregeya Alfred, Dkt. Mukhwana Ayub na Bw. Mungania.

Nawashukuru pia wasomi wenzangu tulioshirikiana na kushauriana nao katika kozi hii. Wao ni Mwenderani Beatrice, Kiongera wa Kiongera, Kiende Ferinda, Kinyaa Jackline, Rori Zipporah, Were Everlyne na Amolloh Shadrack.

Shukrani kwa ndugu zangu John Kimani, Patrick Kimuchu, Mary Kahaki na Angel Uwetonza kwa nasaha na msaada wao wakati wa masomo yangu. Rafiki na dada yangu Teresiah Nungari Wanjema na Ann Wanjiku Mungai walijitolea kwa kunipa ushauri na ufadhili ili kufanikisha kina cha elimu. Mungu awabariki.

Nawatolea shukrani marafiki wote walioniwezesha kufanikisha kazi hii wakiwemo Shitemi Mulama aliyenifadhili kwa ushauri mwingi katika kazi hii, Patriciah Mulyanga, Thiongo Maina, Bascline Mwangi, Martha Kinyua, Meja Dominic Mwose na Paul Jodo. Naomba Mola awashushie na awazidishie baraka zake.

Aidha shukrani ziwaendee walimu ninaofundisha nao Hospital Hill na Tume ya Uwajibiri ya Walimu kwa kunipa fursa hii ya kuendeleza masomo yangu. Shukrani pia ziwafikie marafiki wote ambao sikuwataja. Mungu awabariki.

ORODHA YA VIFUPISHO

Bw. Bwana

Bi. Bibi.

Dkt. Daktari.

Prof. Profesa.

TUKI Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

IKISIRI

Utafiti huu unashughulikia arki za simulizi bunilizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Arki ni sifa za usimulizi wa hadithi bunilizi au halisi. Ni vipengele vya kimuundo ambavyo hutumika kwa njia tofauti tofauti kulingana na usimulizi husika.

Aidha, ni elementi zinazotumika katika usimulizi wa hadithi ili kufanikisha mawasiliano na uelewa wa hadithi husika. Katika utafiti huu tunatumia nadharia ya naratolojia mwegemeo wa Rimmon-Kenan (2002). Tunataka kuchunguza na kuthibitisha kuwa kuna matumizi ya usimulizi katika ushairi kama ilivyo katika riwaya.

Tunaigawanya kazi yetu katika sura sita. Katika sura ya kwanza tunajadili somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

Katika sura ya pili tunashughulikia usimulizi, usimulizi wa hadithi, sampuli za wasimulizi, viwango vya usimulizi, uhusika wa msimulizi hadithini, uhusika na mhusika, wakati wa usimulizi, utegemeo wa msimulizi na hadhi ya msimulizi.

Katika sura ya tatu nayo tunachunguza mpangilio wa matukio katika hadithi ambao umegawanywa katika mikondo mitatu: mpangilio wa matukio katika mfuatano wa wakati, muda katika usimulizi na idadimarudio ya matukio katika hadithi.

Tunahakiki mtazamo katika sura ya nne ambao unachukua sura mbalimbali kama vile sura ya mwanda wakati na mwanda mahali, sura ya saikolojia na sura ya itikadi.

Katika sura ya tano tunashughulikia uwasilishaji wa usemi na mawazo. Tunatalii usemi halisi na mawazo halisi, usemi halisi huru na mawazo halisi huru, usemi taarifa na mawazo taarifa na usemi taarifa huru na mawazo huru. Sura ya sita ni hitimisho la kazi nzima, matokeo ya utafiti na mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI	iv
ORODHA YA VIFUPISHO	vi
IKISIRI	vii

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi	1
1.1 Tatizo la Utafiti.....	2
1.2 Madhumuni ya Utafiti	3
1.3 Maswali ya Utafiti	4
1.4 Sababu za Kuchagua Somo	4
1.5 Upeo na Mipaka	5
1.6 Msingi wa Nadharia	6
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili.....	11
1.8 Mbinu za Utafiti	16
1.9 Hitimisho	16

SURA YA PILI : USIMULIZI WA HADITHI

2.0 Utangulizi	18
2.1. Sampuli za Wasimulizi.....	22
2.2 Viwango vya Usimulizi.....	24

2.3 Uhusika wa Msimulizi Hadithini.....	25
2.4 Uhusika na Mhusika	26
2.4.1 Mhusika	26
2.4.2 Uhusika.....	35
2.4.2.1 Viakisi dhahiri vya uhusika katika matini	35
2.4.2.2 Viashirii vya uhusika visivyodhahiri.....	36
2.4.2.2.1 Matendo	36
2.4.2.2.2 Usemi.....	37
2.4.2.2.3 Muonekano wa nje	38
2.4.2.2.4 Mazingira.....	39
2.4.2.2.5 Mfananisho	39
2.5 Wakati wa Usimulizi	40
2.5.1 Usimulizi Baadaye.....	40
2.5.2 Usimulizi Kabla.....	42
2.5.3 Usimulizi Sambamba.....	43
2.6 Utegemefu wa Msimulizi	43
2.7 Hadhi ya Msimulizi	44
2.8 Hitimisho	46

SURA YA TATU : MPANGILIO WA MATUKIO

3.0 Utangulizi	48
3.1 Mpangilio wa Matukio Katika Mfuatano wa Wakati.....	48
3.1.1 Analepsia	48

3.1.2 Prolepsia	50
3.1.3 Mwanda	52
3.1.4 Masafa	53
3.2 Muda Katika Usimulizi	54
3.2.1 Muhtasari	55
3.2.2 Udondoshi.....	57
3.2.3 Onyesho	58
3.2.4 Mtuu	61
3.3 Idadimarudio/Umara.....	63
3.3.1 Umarudio Mara Moja	64
3.3.2 Umarudio Mara Nyingi	65
3.3.3 Umarudio Sisitizi.....	66
3.4 Hitimisho	67

SURA YA NNE: MTAZAMO

4.0 Utangulizi	68
4.1 Mtazamo Katika Usimulizi.....	69
4.1.1 Sura za Mtazamo	70
4.1.1.1 Sura ya Mwanda Mahali na Wakati	70
4.1.1.2 Sura ya Saikolojia.....	71
4.1.1.3 Sura ya Itikadi.....	72
4.2 Hitimisho	73

SURA YA TANO : UWASILISHAJI WA USEMI NA MAWAZO

5.0 Utangulizi	74
5.1 Usemi Halisi na Mawazo Halisi	75
5.2 Usemi Halisi Huru wa Mawazo Halisi Huru.....	75
5.3 Usemi Taarifa na Mawazo Taarifa	77
5.4 Usemi Taarifa Huru na Mawazo Huru	79
5.5 Hitimisho	79

SURA YA SITA: HITIMISHO

6.0 Utangulizi	81
6.1 Muhtasari wa Matokeo	81
6.2 Mapendekezo.....	86
6.3 Hitimisho	87

MAREJELEO	88
------------------------	-----------

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Utendi wa Mikidadi na Mayasa unasimulia juu ya mashujaa wawili wa kiislamu, Mikidadi na Mayasa na jinsi walivyoshinda pingamizi walizowekewa na baba yake Mayasa ili wasioane. Mikidadi alikuwa mwenye usuli wa familia maskini kwani babake Suwedi katika kufa kwake hakumrithisha chochote. Kwa hivyo, Mikidadi alienda kuishi kwa mjombake aliyeitwa Turadi na kumchungia mjombake mifugo

Mayasa alikuwa bintiye Jabiri mjombake mwingine Mikidadi. Mayasa alipotimia umri wa kuolewa alitoa masharti kwa babake kuwa yeyote ambaye angekuja kumposa, ingembidi kwanza apigane naye. Akimshinda katika vita, basi huyo ndiye angekubali kuolewa naye. Wanaume wengi kutoka familia tajiri na za mbali walikuwa wanataka kumposa kwa sababu ya urembo wake.

Mikidadi alipokuwa akichunga mifugo ya Turadi, aliwaona watu waliokuwa wameuawa na alipofanya uchunguzi aligundua kuwa hiyo ilikuwa kazi ya Mayasa. Mikadadi anajawa na hamu ya kujijaribia bahati yake ili aweze kumuoa Mayasa. Tamima, mamake Mikidadi alidai kuwa Mikidadi ni wa asili ya familia ya kimaskini na pia asiyeweza kumpigania Mayasa. Mikidadi alimrai mjombake amwazime farasi ili aende kupigana na Mayasa. Mikidadi alipoenda uwanjani alikabiliana na waposaji wengine aliowakuta. Mikidadi mwishowe alimshinda Mayasa ambaye alikiri kuwa huyo ndiye mume shujaa aliyetamani maishani mwake.

Jabiri, babake Mayasa aliamua kumtamausha Mikidadi kwa kudai mahari mengi kupindukia lakini Mikidadi aliahidi kulipa hata zaidi. Alipoleta mahari alipata Mayasa ameoza kwa Maliki lakini Mikidadi alipigana na kumnyakua Mayasa. Maliki anapanga njama ya kumuua Mikidadi lakini anaokolewa na Ali na Hamza.

1.1 Tatizo la Utafiti

Utafiti katika tendi za Kiswahili katika karne ya ishirini na moja haujashughulikiwa kwa mapana, kwa hivyo ni vyema kuchukua changamoto na kuendeleza utafiti katika ushairi wa kale. Utafiti huu utachunguza ikiwa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaakisi sifa za simulizi bunilizi kwa sababu wasomi wengi hawakujishughulisha na uhakiki huu wa kinaratolojia katika ushairi wa kale wa Kiswahili.

Wataalamu kama vile Mutiso (1996:2), wanadai:

“Wasomi wengi wa Kiswahili, wanaonekana kupoteza hamu katika fasihi ya Kiswahili ya Kiislamu (kale). Si ajabu imeonekana na kuchukuliwa kama ngeni”.

Ingawa hatuafikiani kikamilifu na maoni ya Mutiso, kwa sababu wengi walishughulikia ushairi wa kale kwa kujikita tu katika tafsiri bila kuhakiki. Baadhi ya watafiti walioshughulikia ushairi wa kale ni wa kigeni nao ni Dammann, (1940), katika *Dichtugen der Lamu Mundert des Suaheli*, Knappert (1964, 1967 na 1979), katika *Four Swahili Epis, Traditional Swahili Poetry* na *Four Century of Swahili Verse*, Werner (1932), katika *Hadithi ya Mikidadi na Mayasa*, Harries (1962), katika *Swahili Poetry* na Allen (1971), katika *Tendi*.

Lengo kubwa la watafiti hawa lilikuwa kutaka kuwafundisha wageni hasa wa kimagharibi kuhusu ushairi wa kale wa Kiswahili. Kwa hivyo kuna pengo kubwa sana katika uhakiki wa ushairi wa kale kwa kutumia nadharia mbalimbali. Jambo hili likawa ni msukumo kwetu kuhakiki ushairi wa kale wa Kiswahili wa *Mikidadi na Mayaya* kwa mkabala wa nadharia ya naratolojia.

Aidha ni wazi kwamba utafiti katika ushairi wa kale umefanywa na wengi hasa wa kisasa lakini ni wachache mno ambao wamejikita katika uhakiki wa kinaratolojia wa tendi na hili ni pengo kubwa katika kukosa kuuwekea misingi ya utafiti wa simulizi bunilizi katika mashairi ya kale ya Kiswahili.

Hali kadhalika watafiti wengi wamejikita katika uhakiki wa riwaya na tamthilia wakitumia nadharia mbalimbali kuliko uhakiki wa ushairi wa kale wa Kiswahili.

Na mwisho tumetambua kuwa kuna uhaba mkubwa sana wa marejeleo ya miswada hasa ya kazi ya kinaratorojia. Kwa hivyo hili ni pengo lingine ambalo tunataka kuliziba.

1.2 Madhumuni ya Utafiti

Tuna dhamira mbili katika utafiti huu;

- i. Kutathmini ikiwa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaakisi arki za simulizi bunilizi katika uwasilishaji wake.
- ii. Kuonyesha arki za kisimulizi zilizojenga *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

1.3 Maswali ya Utafiti

Katika utafiti huu tunataka kuchunguza maswali yafuatayo;

- i. Je, *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaakisi sifa za simulizi bunilizi?
- ii. Ni kwa kiwango gani *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unatumia sifa za simulizi bunilizi.

1.4 Sababu za Kuchagua Somo

Tumechagua *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kwa sababu ni baadhi ya tungo za kale za Kiswahili ambazo hazijahakikiwa kinadharia kuchunguza usimulizi bunilizi wake au miundo yake ya kisimulizi.

Pili, baadhi ya tenzi hizi zimeishia kusahaulika kwa kupuuzwa katika utafiti ilihali zilichangia katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, tunachukua changamoto hii kuendeleza utafiti katika ushairi wa kale. Vile vile tutatajirisha hazina ya historia ya ushairi kwa kurejelea tenzi za kale.

Tatu, uhakiki wa kinaratolojia umekuwa ukifanywa katika kazi za kinathari kama riwaya na wala sio ushairi na wale ambao wametumia nadharia hii ni wachache mno kulingana na tuliyoyasoma. Uhakiki uliofanywa kuhusu utenzi huu ni wa kulinganisha fani yake na ya *Swifa ya Nguvumali* bila ya kutumia nadharia ya kinaratolojia.

Nne, utafiti huu utakuwa changamoto kwa wataalamu wengi wa fasihi kutumia nadharia ya naratolojia katika ushairi wa kale wa Kiswahili kwa vile ni utenzi mmoja tu wa *Siri li Asirali* ambao umehakikiwa kutumia nadharia hii ya naratorojia.

Tano, utafiti unakusudia kuonyesha kuwa vipengele vya naratolojia kama vile simulizi, matukio na usimuliaji kama alivyoainisha Genette (1972), vinapatikana katika ushairi wa Kiswahili kama ilivyo katika riwaya.

Sita, utafiti huu utasaidia kwa kiwango kikubwa kuuelewa muundo wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* hivyo kutajirisha hazina ya historia ya ushairi kwa kurejelea tenzi za kale.

1.5 Upeo na Mipaka

Tutajikita katika matini ya *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Tutahakiki matini hii tukitumia nadharia ya simulizi mwelekeo unaohusishwa na Rimmon-Kenan (2002). Rimmon-Kenan amejenga na kuboresha mawazo ya Gerald Genette ya diskosi simulizi.

Tutasoma nadharia ya naratolojia na *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kando kando kisha kuchunguza ikiwa arki za simulizi bunilizi zimetumika katika utendi huu. Arki tutakazochunguza ni kama vile usimulizi utakaohusisha mada ndogo kama vile usimulizi sampuli za wasimulizi, sifa za usimulizi, uhusiano wa masimulizi na hadithi, viwango au daraja za usimulizi, usimulizi wakati na uhusika na mhusika.

Katika sehemu ya tatu tutashughulikia mpangilio wa matukio katika usimulizi. Haya yanahusu analepsia, prolepsia, aina za umarudio na muda katika usimulizi.

Katika sehemu ya nne tutaangazia mtazamo katika usimulizi, sawia za mitazamo ambazo ni sura ya mwanda wakati na mwanda mahali, sura ya saikolojia na sura ya itikadi.

Aidha arki za simulizi bunilizi zingine katika sehemu ya mwisho ni uwasilishaji wa usemi na mawazo unaohusu usemi halisi na mawazo halisi, usemi halisi huru na mawazo halisi huru, usemi taarifa na mawazo taarifa, usemi taarifa huru na mawazo huru. Tutakuwa tukichunguza ikiwa arki hizi zinapatikana katika *Utendi wa Mikdadu na Mayasa* kama ilivyo katika maandishi ya kinathari kama riwaya.

1.6 Msingi wa Nadharia

Shughuli za kinaratolojia halisi tofauti na za umuundo zilianza kuchukua mkondo mahsusi baada ya 1958, baada ya tafsiri ya Kiingereza ya kazi ya Vladmir (1966), *Morphology of Folktale*, ya Levi (Fokkema 1997). Kama somo, naratolojia ilianza 1966 baada ya uchapishaji wa makala maalum "*Communications*" yaliyotengewa uchambuzi wa hadithi kimuundo. Waliochangia katika makala haya ni kina Greimas, Genette, Barthes, Bremond na Todorov na ndio waasisi wa naratolojia.

Prince katika Seldan (1985) ameeleza kuwa kihistoria nadharia ya naratorojia imechipuka kutoka umuundo wa Kifaransa. Vile vile Davis na Schleifer (1996) wameonyesha umuhimu wa umuundo katika kukuza naratolojia kwani umuundo wao

ulijaribu kuchanganua muundo wa hadithi. Prince anaendelea kueleza kuwa naratolojia inachunguza sifa za simulizi zote na zile zinazoweza kuitwa simulizi pamoja na kile kinachoweza kutofautisha simulizi hizi miongoni mwa nyingine. Lengo lake kubwa ni kutenganisha mifumo muhimu ya kaida za simulizi zinazoweza kutolewa simulizi na uundaji wake.

Genette (1972) ni miongoni mwa wananaratolojia wa kirasimi ambao waliweka misingi ya nadharia ya naratolojia. Genette anaainisha hoja tatu kuu katika kuelezea dhana ya simulizi. Dhana hizi ni kutoa maelezo ya kauli ya kisimulizi iliyokusudiwa kulieleza tukio au matukio fulani ambayo ni dhana ya simulizi, usimuliaji ambao unaelezea tendo lenyewe la kusimulia au usimulizi na kurejelea mfuatano wa matukio halisi au ya kibunilizi ambayo ni kiini au yanayolengwa na usemi fulani ambayo ni dhana ya hadithi au daigesia. Daigesia ni mbinu ya kusimulia hadithi bila kuhusisha kuonyesha vitendo wala usemi.

Mawazo haya ya Genette yanafanana na ya Plato katika andiko lake maarufu *Republic* lililodhihirisha kuwa msingi wa mawazo ya naratolojia. Anatoa maoni muhimu kuhusiana na usimuliaji ambao anaulinganua na udhihirishaji. Mawazo hayo yanafumbatwa na dhana mbili za kimsingi mimesia na daigesia kama alivyoelezea Genette. Katika daigesia mshairi au mtunzi anajitokeza wazi wazi. Yeye ni msemaji anayeweza kutambulika ili hali mimesia mshairi hajitokezi kama msemaji na hivyo amefichika.

Wamitila (2005:140), anaeleza:

“Suala moja muhimu katika ukuaji wa nadharia hii ni kutambua na kukubaliana kuwa simulizi na hadithi hutambwa kwa njia mbalimbali kwa matumizi ya nathari au ushairi, ikiwa andishi au simulizi. Hali kadhalika matukio yanaweza kuwasilishwa kwa jinsi mbalimbali.”

Ufafanuzi huu wa Wamitila unachangia pakubwa uelewa wa kutofautisha naratolojia kwa jumla na naratolojia bunilizi. Naratolojia kwa jumla inaweza kutumiwa nje ya mipaka ya fasihi kama vile kuhusisha vitabu vya kihistoria, densi, mchezo-bubu, ripoti za magazeti na filamu kwa mujibu wa Rimmon-Kenan (2002).

Naratolojia bunilizi inahusisha mfuatano wa matukio ambayo yanaweza kuwa ya kibunifu au halisi lakini tukio moja haliwezi likatolewa ufafanuzi huu. Hata hivyo matukio yanayopatikana katika matini hayafuatani kiwakati. Hali hii inasababishwa na mbinu za kisimulizi kama analepsia na prolepsia. Matukio yanayosimuliwa huweza kudhihirishwa au kuwasilishwa kwa njia mbalimbali ambazo ni uelezaji na uonyeshaji.

Dhana hizi mbili zimefumbatwa na istilahi za Plato, daigesia na mimesia. Hivyo basi msimulizi anaweza kusimulia au kuelezea matukio baada ya kutokea (analepsia) na ndiyo hutumika sana au kusimulia kabla ya kutokea kwake (prolepsia). Huu ndio mtindo wa kisimulizi ambao Prince anaelezea kama ‘usimulizi wa kitabiri’. Mtindo huu haupatikani kwa kawaida katika uandishi wa kibunilizi. Aina ya tatu ni usimulizi ambao

matukio yanasimuliwa wakati huo huo wa kutokea yaani ‘usimulizi mtawalia’ lakini hutumika hasa katika sanaa za kiutendaji kama drama au filamu.

Rimmon- Kenan (2002) anaielezea hadithi kama matukio yaliyosimuliwa yakiondolewa katika matini na kuungwa katika mfuatano wake wa kiwakati. Neno ‘matini’ linarejelea kile ambacho tunakisoma na inakaribiana na jinsi linavyotumiwa katika uhakiki wa kisimiotiki yaani jinsi kazi za fasihi zinavyowasiliana na wasomaji. Kulingana na maelezo hayo maswala makuu katika usimulizi ni wakati, wakala (ajenti) wa usimuliaji, mkabala wa kimtazamo na usemi au diskosi.

Wakati ni muhimu sana kwa vile matukio yoyote yale hutendeka katika wakati maalum. Hivyo wahakiki wa kinaratolojia hubainisha kati ya ‘wakati-hadithi’ na ‘wakati-matini. Wakati-hadithi ni muda uliotumika katika kusimulia hadithi na wakati–matini ni muda uliotumika katika kutendeka kwa matukio katika matini’. Muda wa wakati-hadithi huwa mfupi kuliko wa hadithi-matini, basi mwananaratolojia sharti achunguze kilichosimuliwa, matukio yaliyosimuliwa na usimuliaji wenyewe na njia iliyotumiwa.

Manfred (2005) amejadili kuhusu mwongozo wa nadharia ya usimulizi huku akishughulikia mada kama vile: tanzu za simulizi, daraja au viwango vya usimulizi, usimulizi sauti, usimulizi damisi au mahasa (mood) baadhi ya mada nyingine. Kazi hii ya Manfred itachangia kazi yetu sana ya kuhakiki *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kwa sababu tutachunguza iwapo elementi hizi zinapatikana katika utendi.

Guillemette na Levesque (2006), katika diskosi simulizi wamejadili juu ya usimulizi hali (narrative mood), uhusiano wa msimulizi na hadithi, viwango au daraja za usimulizi, usimulizi wakati (Narrative time) baadhi ya mada nyingine. Katika kazi yetu tutashughulikia baadhi ya mada hizi za Guillemette na Levesque katika kuhakiki *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

Greimas (1966) naye katika uandishi wake anashughulikia muundo wa ndani wa usimulizi. Anashughulikia sarufi katika usimulizi akiegemea sana nadharia ya Simiotiki na uhusiano wa usimulizi katika tajriba zote. Hali kadhalika ameshughulikia uhusika na nafasi ya mhusika kwa kina katika usimulizi. Amedhihirisha kuwa hatuwezi kushughulikia usimulizi bila kujumuisha uhusika na mhusika pamoja. Kazi ya Greimas ina manufaa sana katika kuelewa msingi wa nadharia ya naratolojia ambayo inahusu muundo kwa kiasi kikubwa.

Kulingana na Barthes (1970) anaeleza kuwa simulizi zote zina vipengele vya muundo ambavyo hutumika kwa njia tofauti kulingana na usimulizi. Licha ya simulizi hizi kutofautiana kimuundo kila simulizi hutumia mfumo au utaratibu wa muundo unaoathiri usomaji wa matini. Anaelezea kuwa hii ni changamoto ya kumwezesha msomaji kutumia kanuni zinazomsaidia kuelewa na kuchanganua maana tofauti zinazojitokeza katika matini.

Ni muhimu kutambua kuwa kutokana na usomaji wetu nadharia ya kinaratolojia ina vipengele vingi vya kuhakikiwa katika tenzi za kale za Kiswahili, kazi za kitafiti katika

ushairi wa kale wa Kiswahili ni chache sana na nadharia ya naratolojia imetumiwa na msomi mmoja tu katika kuhakiki utenzi wa *Siri li Asirali*. Kwa hivyo kulingana na maoni yangu hii ni kazi ya pili katika kuhakiki utendi wa kale wa kiswahili katika kiwango cha uzamili katika misingi ya naratolojia.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili

Tafiti kadha zimefanywa kuhusu tenzi za Kiswahili. Waliofanya utafiti katika enzi za kale ni pamoja na Knappert (1967, 1971, 1979), aliyeshughulikia tenzi nyingi kama vile kufufua *Utenzi wa Ayi Wangi Wangi* uliokuwa umefifia au kupotea, alichunguza Uislamu wa Afrika Mashariki unavyoakisiwa katika tenzi za Kiswahili, akaelezea umuhimu wa kuthamini mashairi ya Kiswahili baadhi ya kazi nyingi alizofanya. Kwa mujibu wa Hichens, kama alivyonukuliwa na Knappert (1979:66), Fumo Liyongo aliishi kabla ya mwaka 1230 Masihia, mwaka ambao Mfalme wa kwanza wa Pate alitekwa nyara mji wa Shaga alimoishi Liyongo. Knappert anaendelea kueleza kwamba Fumo Liyongo na Aldarusi ni miongoni mwa walumbi mashuhuri wa Waswahili. Fumo alitunga nyimbo kadhaa za ushairi ndiposa anakumbukwa hadi leo.

Allen (1971), naye alishughulikia tafsiri za tenzi kama vile *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kutoka Kiswahili hadi Kiingereza. Tafsiri ya Allen inatusaidia katika kuelewa utendi huu kwa kina. Lambert (1965), naye alijikita katika kuuchunguza *Utenzi wa Mwana Mnga* na Harries (1962), alishughulikia mashairi ya Kiswahili kama vile *Ayi Waji Waji* na *al-Inkishafi* (1972). Hao ni miongoni mwa wengine wengi.

Baadhi ya tenzi zilizotungwa zilikuwa ndefu mathalani *Utenzi wa Siri li Asirali, Rasil-al-Ghuli* na *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Tenzi zina sifa za kipekee ambazo huzitofautisha na mashairi ya kisasa na maandishi mengine.

Lengo kubwa la watafiti hawa wageni lilikuwa kuwafundisha wageni wa kimagharibi kuhusu ushairi wa kale na ndivyo wengi wakajikita katika tafsiri pekee. Haya yamepelekea baadhi ya wasomi wa fasihi ya Kiswahili kupuuza mchango wa watafiti hawa katika fasihi ya Kiswahili. Kezilabahi, (1997:59) anaeleza:

“...wale wataalamu wa kizungu ambao wamejitahidi sana kukiendeleza na kukikuza Kiswahili walikuwa na ujuzi mdogo sana wa fasihi. Wao walikuwa wataalamu wa lugha na hawakuweza kufanya lolote zaidi ya kukusanya maandishi kadha ya Kiswahili na kuyatafsiri katika lugha zao kwa manufaa yao wenyewe.”

Hata hivyo watafiti hao walichangia pakubwa katika kuweka misingi ya utafiti katika tenzi za kale za Kiswahili.

Mbali na watafiti wa kigeni uhakiki umefanywa hivi majuzi kuhusu tenzi za kale na wasomi kama vile Mutiso (1985,1996, 2003, 2005), Olali (2004), Mungai (2005), Shitemi (2011), Murage (2011) miongoni mwa wengine. Utafiti wetu unahusu *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na utashughulikia mambo matatu makuu. Moja ni usimulizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, pili nadharia ya naratolojia na tatu matini ya utendi wenyewe. Tulisoma kazi zinazohusu naratolojia na tukapata kwamba hakuna

utafiti wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* uliohakikiwa kutumia naratolojia. Kazi ambayo imeshughulikiwa ya kinaratolojia ni katika *Utendi wa Siri li Asirali* na Shitemi (2011). Ingawa msomi mwingine aliyehakiki *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni Mungai (2005), katika ulinganishi wa kifani na *Swifa ya Nguvumali* kwa kutumia nadharia ya urasimi inayoangalia fasihi kama sanaa ya maneno. Amelinganisha sifa za fani kama vile, wahusika mtindo, muundo, toni na mandhari. Kazi ya Mungai itatufaa sana katika kuelewa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* hasa katika uhusika na mtindo ingawa nitajikita katika simulizi bunilizi mwelekeo wa Rimmon-Kenan (2006) wa naratolojia.

Mungai katika kazi hii yake hata hivyo hakushugulikia usimulizi ambao utafiti huu unaazimia kuziba. Amelinganisha fani na vipengele vyake katika tenzi hizi mbili kwa kutambulisha kila mojawapo na kuchanganua maana na uamilifu wake katika muktadha wa matumizi lakini utafiti wetu utajikita katika utendi uu huu bali tutashughulikia usimulizi bunilizi.

Rimmon-Kenan (2002), ameshughulikia vipengele vya naratolojia vya matokeo na wahusika katika hadithi, usimulizi na uwasilishaji wa matini za fasihi, sauti na viwango katika usimulizi, wakati katika matini, mtazamo katika matini na mikondo ya nadharia ya naratolojia. Utafiti wetu unatumia nadharia hii ya naratolojia ya Rimmon-Kenan ambayo inatufaa sana. Ingawa kazi yetu mbali na kuchunguza hayo yaliyoshughulikiwa na Rimmon-Kenan tutatalii uhusika na mhusika katika hadithi.

Mtaalamu ambaye ametuwekea msingi wa kuhakiki tendi za kale za Kiswahili ni kama tulivyotaja hapo juu Mutiso (1995), aliyeshughulikia maudhui ya hurafa na uyakinifu katika *Utenzi wa Hamziyyah*. Katika kazi hii amelinganisha sifa apewazo Mtume Mohammed na zile za mashujaa wengine duniani kwa kutumia nadharia ya umaksi. Aidha ameifasiri kasida yote kwa Kiswahili na kufafanua mtindo wa utendi huu. Vile vile ametafsiri *Kasida ya Hamziyyah* kwa Kiingereza.

Ametafsiri *Kasida ya Burudai* (1996), kwa Kiingereza na Kiswahili. Pia amehakiki kwa misingi ya *Archetypal motifs* kwa kushughulikia suala la fasihi zilizo na misingi ya kiislamu. Utafiti wetu unatofautiana na kazi ya Mutiso kwa vile tutajikita katika simulizi bunilizi katika utendi wa Mikidadi na Mayasa.

Naye Olali (2004), ameendeleza kazi ya Mutiso (1985) ya uhakiki wa *Kasida ya Hamziyyahi* ingawa kazi yake inajikita sana katika drama kuliko ushairi. Alishughulikia maudhui katika *Hamziyyah* na jinsi yanavyochangia katika kumtukuza Mtume Mohammed wakati wa Maulidi ya Lamu Kisiwani. Pia ameambatisha kiambatisho cha *Utenzi wa Hamziyyah* sura ya 4 katika tasnifu yake ya uzamifu. Utafiti wetu utajikita katika usimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* tofauti na uchunguzi wa elementi za drama kama alivyofanya Olali. Hata hivyo kazi ya Olali imetuwekea msingi wa elementi tutakazotalii katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kama vile uwasilishaji wa usemi ambapo katika drama usemi ni kipengee muhimu sana.

Shitemi (2011) katika tasnifu yake ya uzamili ameshughulikia usimulizi katika *Utenzi wa Siri li Asirali*. Kwa mujibu wa msomi huyu ameshughulikia mada zinazoendelezwa kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Ametumia vipengele vikuu vya diskosi simulizi kama vilivyoelezwa na Genette (1972). Vipengele hivi ni usimulizi, aina za wasimulizi, viwango vya usimulizi na sifa za usimulizi. Aidha ametumia vipengele vya wakati wa usimulizi, kuonekana kwa msimulizi, hadhi ya msimulizi, umarudio wa usimulizi, hali ya usimulizi na sauti ya msimulizi.

Shitemi vile vile ametumia vipengele vya uwasilishaji wa usemi na mawazo kama ilivyoelezwa na Wamitila (2008). Ameshughulikia usemi halisi na mawazo halisi, usemi halisi huru na mawazo halisi huru, usemi taarifa na mawazo taarifa na usemi taarifa huria na mawazo huria katika *Utenzi wa Siri li Asirali*. Katika utafiti wetu wa arki za simulizi bunilizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* tutatumia baadhi ya vipengele ambavyo Shitemi ametumia katika kazi yake.

Shitemi (2011:9-10) anaeleza:

“.....Diskosi simulizi ni kiunzi cha nadharia ya naratolojia ya fasihi ambayo inaweza kutumiwa kueleza orodha nzima ya mikakati ya simulizi zilizoko. Kila matini inadhihirisha chembe za usimulizi ambazo zinaweza kuchunguzwa ili kuelewa mpangilio wa simulizi”.

Maelezo ya Shitemi yanatufaa sana katika kazi yetu kwa sababu diskosi simulizi ndio msingi wa naratolojia, nadharia ambayo tutaitumia kuuhakiki *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, tukifuata mkondo uliochukuliwa na Rimmon-Kenan (2002) wa simulizi bunilizi.

1.8 Mbinu za Utafiti

Kimsingi utafiti huu utakuwa wa maktabani. Tumesoma mashairi na tenzi mbalimbali za kale na tukateuwa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* miongoni mwa tenzi nyingi za Kiswahili kama vile:

Al Inkishafi, Miraji, Liyongo, Kiokozi cha Banati, Mwanananga, Ayi Waji Waji, Wangi Wangi, Ayubu, Rasil LGhuli, Siri li Asirali, Siu, Utendi wa Mwana Kupona na Fatuma miongoni mwa nyingine nyingi.

Tutasoma *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kwa kina ili tuainishe na kufafanua sifa za simulizi bunilizi zilizotumika kama ilivyo katika riwaya kwa kutumia nadharia ya naratolojia mwegemeo wa Rimmon-Kenan (2002).

Tutadurusu tasnifu mbalimbali zinazohusu ushairi, vitabu, majarida na machapisho mengine ambayo yana makala yaliyo na manufaa katika utafiti wetu. Tarakilishi ni nyenzo muhimu sana katika utafiti na hivyo tutatumia mtandao kama njia ya pili ya kufanyia utafiti wetu. Tatu, tutapata ushauri kutoka kwa wahadhiri wetu, wataalamu wa utanzu huu wa fasihi na wanafunzi wenzangu.

1.9 Hitimisho

Katika sura hii ya kwanza, tumeshughulikia muhtasari wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Utendi unahusu vita vya Mayasa na Mikidadi kulingana na masharti ya Mayasa kuwa angeolewa na mwanamume ambaye angemshinda katika vita hivyo. Tumejadili tatizo la utafiti, madhumuni ya tasnifu hii, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada

ya kuchunguza arki za simulizi bunilizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na upeo na mipaka ya kazi hii. Msingi wa nadharia ya naratolojia kulingana na Rimmon-Kenan (2002) na waandishi wengine kama vile, Genette (1972), Manfred (2005), Greimas (1996), Guillemette na Levesque (2006), Barthes (1970) na Wamitila (2005), umeshughulikiwa kwa kirefu kwa vile ndio utatumika kuhakiki utendi huu wa kale wa Kiswahili. Kisha tukachunguza yaliyoandikwa kuhusu somo hili, mbinu za utafiti na mwisho ni hitimisho.

SURA YA PILI

USIMULIZI WA HADITHI

2.0 UTANGULIZI

Sura hii itamulika hadithi ya Mikidadi na Mayasa, usimulizi wa hadithi, sampuli za wasimulizi, viwango vya usimulizi, uhusika wa msimulizi katika hadithi, usimulizi wa matukio, utegemevu wa msimulizi na hadhi ya msimulizi. Aidha tutachunguza kipengele cha uhusika na mhusika kinachofafanua makundi ya wahusika kama alivyoelezea Greimas (1966) na uhusika kama sehemu ya hadithi kulingana na Rimmon-Kenan (2002). Kabla ya kuchunguza arki hizo za simulizi bunilizi katika kazi hii ni vyema kundokeza *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ili kuchangia katika uelewa wa mifano katika kuthibitisha arki zilizotumika.

Utendi wa Mikidadi na Mayasa ulitungwa na Said Abdallah Masudi el Bulhry miaka mingi kabla ya karne ya ishirini. Umetafsiriwa kwa Kiingereza na Allen, (1971). Utendi huu umehakikiwa na Mungai, (2005) katika ulinganishi wa kifani na *Utendi wa Swifa ya Nguvumali*.

Utendi wa Mikidadi na Mayasa unasimulia juu ya mashujaa wawili wa kiislamu, Mikidadi na Mayasa na jinsi walivyoshinda pingamizi walizowekewa na baba yake Mayasa ili wasioane.

Mikidadi alikuwa mwenye usuli wa familia maskini kwani babake Suwedi katika kufa kwake hakumrithisha chochote kama tunavyoarifiwa katika utendi. Suwedi alikuwa tajiri

lakini mali yote yaliishia katika safari nyingi alizosafiri. Tunaarifiwa kuwa hakuwa hata na mke kwa sababu ya unyonge wake.

Baada ya kifo cha Suwedi babake Mikidadi, Mikidadi alienda kuishi kwa mjombake aliyeitwa Turadi Bin Annan. Alifanya kazi ya kumchungia mjombake mifugo kama vile mbuzi, ng'ombe na ngamia.

Mayasa alikuwa bintiye Jabiri mjombake mwingine Mikidadi. Mayasa alipotimia umri wa kuolewa alitoa masharti kwa babake kuwa yeyote ambaye angekuja kumposa, ingembidi kwanza apigane naye. Akimshinda katika vita, basi huyo ndiye angekubali kuolewa naye. Mayasa alikuwa amepigana na wanaume wengi na baadhi yao wakauawa na wengine kutoroka kwa kuhofia kifo au kushindwa katika vita hivyo.

Mayasa alikuwa mrembo sana na kwa hivyo sifa za urembo wake zilifika mbali. Wanaume wengi kutoka familia tajiri na za mbali walikuwa wanataka kumposa kwa sababu ya urembo wake.

Mikidadi alipokuwa akichunga mifugo ya Turadi, aliwaona watu waliokuwa wameuawa na alipofanya uchunguzi aligundua kuwa hiyo ilikuwa kazi ya Mayasa. Hivi ni kulingana na masharti aliyokuwa ameweka ya kuolewa na shujaa wa kumshinda vitani. Mikadadi anajawa na hamu ya kujijaribia bahati yake ili aweze kumuoa Mayasa.

Tamima, mamake Mikidadi alimkaripia mwanawe asijitome kwenye vita vya Mayasa baada ya Mikidadi kumwelezea Tamima msimamo wake kuhusu kujaribu bahati yake ya kumuoa msichana huyu. Tamima naye anamshauri mwanawe kwa yale ambayo wameyashuhudia kuhusu vita vya Mayasa na wanaume wengine ambao ni matajiri wa kutajika ilihali hawakuweza kufaulu kumuoa Mayasa.

Tamima alidai kuwa Mikidadi ni wa asili ya familia ya kimaskini na pia asiyeweza kumpigania Mayasa. Mikidadi alimrai mjombake amwazime farasi ili aende kupigana na Mayasa. Mikidadi alipoenda uwanjani mwa vita alikabiliana na waposaji wengine aliowakuta. Aliwaua wengi na wengine wakatoroka. Jaribio hili lilimpendeza Mayasa na akatamani wapigane na shujaa huyo aliyepigana kiajabu.

Vita baina ya Mikidadi na Mayasa vilikuwa vikali kila mmoja akijitahidi kumshinda mwenziwe. Kadri walivyopigana ndivyo hisia za mapenzi zilivyozidi baina yao. Mikidadi mwishowe alimshinda Mayasa ambaye alikiri kuwa huyo ndiye mume shujaa aliyetamani maishani mwake.

Jabiri, babake Mayasa aliamua kumtamausha Mikidadi kwa kudai mahari mengi kupindukia. Jabiri alifanya hivi kijeuri akijua kuwa haingewezekana katika muda wa miezi mitatu kupata mahari hayo yote - ngamia arobaini, ngombe hamsini, farasi weusi mia moja, nguo mia saba, farasila na dhahabu (ubeti wa 147-152).

Turadi, mjombake Mikidadi aliyaona mahari yenyewe kuwa mengi zaidi ya uwezo wao kupata lakini Mikidadi aliahidi kuwa angeleta yote na hata kuongeza zaidi. Mikidadi aliondoka kwao na kwenda mwendo mrefu miambani kwenye njia za kupitiwa na wasafiri na wafanyibiashara. Ikawa kila anayepita anamshambulia, kupigana vita vikali, kuuu na kunyang'anya mali yote. Alifanikiwa kupata mali mengi lakini alipoamua kurudi kupeleka posa, alipata habari kuwa Jabiri alimuoza Mayasa kwa Sultani Maliki bin Riyabi. Mikidadi alikutana na washenga wa Maliki na kishujaa alipigana nao na kumpata Mayasa.

Mbali na hayo kulizuka vita baina ya Ali na Mikidadi kutokana na Mayasa kutaka Fatuma apokonywe taji. Mwishowe Ali alimshinda Mikidadi na kumsilimisha. Mayasa na Mikidadi wanaandamana hadi nyumbani kwa Jabiri kwa njia za hila na kutaka Jabiri kumrejeshea Maliki mahari aliyopokea. Jabiri anamfahamisha Maliki kuhusu jinsi Mikidadi alivyowashambulia watumishi wake na kumchukua Mayasa kama mke. Kwa pamoja, njama ilipangwa na Maliki na jeshi lake ili kumwadhibu Mikidadi kwa kifo hivyo, wakamfunga na kupanga mauaji kesho yake.

Mikidadi alimuuliza mamake ajikaze na kuomba Mola ili kumnusuru kifo hiki. Tamima alipotoka, malaika Jibrili akashuka na kuandamana naye hadi kwa Mtume Mohammed. Kisha Mungu akamtuma malaika Mikaili aiharakishe safari ya Tamima kwa kuikunja ardhi ili Tamima afike haraka Medina. Alipofika alimpata Mtume amesimama mlangoni anamsubiri kwa vile Mtume alikuwa amearifiwa na Malaika Jibrili na Hamza akatoka kukutana na Tamima. Tamima akamwarifu Mtume juu ya mtoto wake Mikidadi

alivyokuwa amefungwa na jeshi la Maliki. Kisha Mtume akamtuma Hamza kumwita Ali na alikuwa aje akiwa amejihami na zana za vita ili kukabiliana na Maliki na Jabiri.

Ali alipofika alipata kuwa nyumba ya Mikidadi ilikuwa imezingirwa na askari zaidi ya mia mbili. Ali na Hamza walipigana vita vikali na kumwokoza Mikidadi huku wakimuuua Maliki na kukata kichwa chake. Mikidadi aliandamana na Ali kwenda kwa Mtume huku Medina ili kupigana katika vita vya jihadi na walipofika kwa Mtume waliandaliwa karamu kubwa sana kwa ushidi wa Mikidadi.

2.1. Sampuli za Wasimulizi

Wananaratolojia kama Rimmon-Kenan (2006), wanasema wasimulizi wa hadithi hupatikana katika makundi kadhaa kwa kutegemea vigezo viwili; daraja ya hadithi anayoesimulia msimulizi na ushiriki wa mhusika katika hadithi anayoisimulia. Kwa kurejelea kigezo cha daraja, kuna aina mbili za wasimulizi. Wasimulizi hawa ni wasimulizi nje na wasimulizi ndani katika hadithi wanayoisimulia.

Msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* anaakisi kwa kiwango kikubwa msimulizi nje. Katika hadithi anayoisimulia haonyeshi kushiriki katika matukio yake.

Katika ubeti 12 msimulizi anasema;

Mbwene hadithi kitabu,

Hadithi hiyo ajabu

Yandishiwe Kiarabu

Njema mno ya ajaa

Fasiri ya ubeti huu ni kuwa hadithi anayoisimulia si utunzi wake. Bali alitafsiri kutoka kitabu kilichoandikwa kwa lugha ya Kiarabu.

Katika ubeti 442, anaendelea kutumia viambishi vya nafsi ya tatu, vinavyorejelea na kuakisi usimulizi nje. Kwa maneno:

Akarudi kwa kisiri,
Ili kumpa khabari,
Mambo yaliyokujiri
Yote kamhadithia

Usimulizi huu unatamalaki *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Hata hivyo, ruwaza hii inakiukwa katika fomula ya ufunguzi na kufunga utenzi ambayo ni kaida katika utenzi wa tenzi kuwa msimulizi anajihusisha kwa kuomba Mola na kumshukuru kwa kumpa maarifa ya kutunga utenzi huu. Hivyo ubeti 1-11, ni utangulizi ambao una uamilifu wa fomula funguzi. Katika ubeti 11, anatamatisha kwa kusema hataki kuendelea sana ila kumwomba Mola amsaidie kuisimulia.

Taiwakifu dibaji
Kwenda mno sihitaji
Nataka omba mpaji
Hadithi kuwasomea

Aidha, katika kufunga utenzi, katika ubeti 778 anajitambua kwa majina na kusema kwamba yeye ndiye amekariri utenzi huo na amefikia kikomo.

Nami mwenye kuradidi,

Isimu yangu Saidi,


Wa Abdala Masudi

Jina langu nawambia

Kwa hivyo, *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* unaonyesha usimulizi nje pakubwa isipokuwa katika fomula funguzi na fomula ya kufunga ambapo msimulizi anajihusisha katika hadithi kwa kutumia nafsi ya kwanza.

2.2 Viwango vya Usimulizi

Wanaratolojia kama Rimmon-Kenan (2006), wanasibisha viwango vya usimulizi na viwango vya hadithi. Hadithi inaweza kuwa na hadithi nyingine. Kwa mfano, mhusika anaweza kusimulia hadithi nyingine katika hadithi kuu. Hivi vijihadithi vinaunda daraja za usimulizi. Yaani hadithi kuu A ikasheheni vijihadithi B na C.



Katika usimulizi wa *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, kiwango kinachojitokeza ni cha kiwango cha hadithi kuu. Hadithi ambayo inahusika hapa ni kuwa; masharti ya ndoa ya Mayasa, vita vya Mayasa na Mikidadi, masharti ya mahari ya Mayasa, utafutaji wa mahari kwa Mikidadi, vita vya Mikidadi na Ali kuhusu taji ya Fatuma, kusilimu kwa Mikidadi, njama ya mjomba wa Mikidadi kumuoza Mayasa kwa Maliki, kutekwa nyara kwa Mikidadi na kuokolewa kwa Mikidadi na Sheikh Ali baadhi ya matukio makuu katika hadithi. Kwa muhtasari msimulizi anasimulia kwa kiasi kikubwa yanayohusu wahusika wawili wanaotamalaki hadithi nzima ambao ni Mikidadi na Mayasa. Hali kadhalika kuna vijihadithi vidogo vinavyojitokeza kama hadithi ya Luhani na Anasa na Kesi. Kutokana na mchoro wetu basi hadithi ya Mikidadi na Mayasa (A) ni hadithi kuu na hadithi ya Luhani na Kesi na mkewe Anasa ni vijihadithi (B) ambavyo vimeegemezwa kwenye hadithi kuu.

2.3 Uhusika wa Msimulizi Hadithini

Swala la uhusika wa msimulizi hadithini unaainishwa kwa mujibu wa daraja za hadithi. Msimulizi wa hadithi kuu ndiye msimulizi wa daraja ya kwanza. Kwa kurejelea uweko au kutokuweco kwa msimulizi hadithini, msimulizi wa daraja ya kwanza ni msimulizi nje. Msimulizi wa daraja ya pili, tatu na kuendelea ni msimulizi wa ndani. Kwa hivyo, anakuwa wa daraja ya pili, tatu na kadhalika.

Kama ilivyo, katika sampuli za wasimulizi, msimulizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni wa daraja ya kwanza. Hii ina maana kuwa, anasimulia hadithi kuu. Kwa hivyo ni mhusika nje. Hata pale, anapoonekana na kujihusisha katika hadithi katika

fomula ya kufungua na kufunga utenzi, kwa hakika si sehemu ya hadithi ni sehemu ya matini tu, ama diskosi.

2.4 Uhusika na Mhusika

Rimmon-Kenan (2002) amedhihirisha utata unaozunguka kipengele cha mhusika katika naratolojia. Rimmon – Kenan anadai kuwa karne ya kumi na tisa, ilishuhudia kutangaza kifo kwa tanzia hali kadhalika kwa mhusika. “Kifo” hapa kinaeleweka kama kupuuzwa katika nyanja za usomi.

Maoni ya Rimmon-Kenan tunayapinga kwa msingi kuwa, licha ya ukuruba wa vipengee hivi katika naratolojia vinachunguzwa chini ya mada mbili tofauti za naratolojia. Yaani mhusika anajadiliwa chini ya mada ya hadithi nao uhusika chini ya mada ya matini. Kutofautisha huku ambako hakuna misingi ya ungavu inazua mtafaruku. Kama tutakavyoonyesha huwezi kuzungumzia mhusika pasi na kuguzia uhusika wake.

Ni vyema ilieweke kuwa vipengele vitatu vya nguzo ya naratolojia ni hadithi, matini na usimilizi (baadhi huiita diskosi). Katika sehemu hii tutajadili vipengee hivi vya naratolojia, kwanza mhusika na pili uhusika.

2.4.1 Mhusika

Kama tulivyokwisha eleza hapo awali kipengee hiki kimepuuzwa katika usomi wa naratolojia. Hata hivyo, Greimas, Barthes na Genette; wananaratolojia wakongwe walijibiidisha kukijadili na kukiweka wazi.

Miongoni mwao, Greimas alijenga kiunzi kizima cha nadharia ya mhusika chini ya naratolojia. Licha ya kuwa wanaratolojia wa baadaye, akiwemo Rimmon – Kenan (2002) wamepuuza kipengee hiki, tunasisitiza kuwa ni muhimu na sharti kishughulikiwe kwani hakuna hadithi bila ya mhusika.

Mawazo ya Greimas kuhusu mhusika yana mantiki. Kwa hivyo, tutayaangalia hapa. Greimas aligawa wahusika katika makundi sita, ambayo yanaweza kuwa binadamu au vitu visivyo na uhai kwa mfano dhana au hirizi za kichawi. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* arki ya makundi haya ya wasimulizi yametumika. Mfano wa wahusika dhana ni matumizi ya malaika Jibrili na Mikaili ambao walitumiwa na Mungu kumuokoa Mikidadi kwa njia za kichawi ambapo ardhi ilijikunja ili safari ya Tamima iharakishwe kufika kwa Mtume Mohamed. Mtume naye alituma kikosi cha jeshi pamoja na Ali ili kumuokoa Mikidadi. Beti zifuatazo zinaelezea haya ;

Tena Rabi kamtuma

Mikaili shuka hima

Ajuza enda kwa Tumwa

Upesi kusikilia (ubeti 697)

Na nti ikundekunde

Safari yake enende

Pasipate muda punde

Madina akatokea (ubeti 698)

Katika makundi haya sita ya wahusika alitambua: mtumwa, kifaa, mpokezi, msaidizi, nguli na mpinzani. Yaani nguli (mhusika mkuu) anataka kitu (kifaa) kilicho na mtu mwingine (mpokezi), katika kusaka kifaa anafanya ushirikiano na mtu mwingine (msaidizi) kukisaka kinachotamaniwa. Nguli huyu anaweza kuwatumia watu wengine kukileta kifaa (mtumwa) akilete mwenyewe. Hata hivyo, kunaye mtu mwingine anayegombea kifaa hicho (mpinzani) ambaye anafanya kupatikana kwake kuwa kugumu. Kunatokea mashindano na hivyo wahusika wanaendeleza hadithi.

Kwa mujibu wa kiunzi hiki, wahusika wengi ama mmoja wanaweza kutekeleza dhima (mhusika) moja. Vile vile, wahusika wanaweza kubadilishana dhima ya mhusika. Kwa mfano, Ayubu na Yusufu wanampenda Njeri. Ayubu na Yusufu katika nyakati tofauti watapata dhima ya mhusika nguli na mpinzani naye Njeri ni kifaa. Ikiwa Yusufu na Ayubu watapigana makonde kwa sababu ya Njeri, kila mmoja atapata dhima ya mpokezi wa makonde kwa zamu yake.

Dhima hizi za mhusika zinaweza kutumiwa kuchanganua *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Mwanzoni mwa utenzi kutoka ubeti 13 hadi 582, Mikidadi ndiye nguli. Anataka ndoa na Mayasa. Mayasa ndiye kifaa ambacho mjombake hataki kumwoza Mikidadi Mayasa kwa sababu za ufukara. Mjombake Mikidadi ni mpinzani. Aidha, watakaokuja kumposa Mayasa wote wakiwemo Warabu wenye mali na Bin Maliki aliyefanikiwa hata kumwoa Mayasa japo shingo upande, kwa amri ya mjombake Mikidadi ni wapinzani. Katika mizani hiyo Bin Maliki anapata dhima ya mpokezi, yaani anacho kile Mikidadi anawania na haiwi rahisi kupokewa inabidi kupiganwe vita ili Mikidadi apate mke.

Mamake Mikidadi (Tamima) anachukua jukumu la kuwa msaidizi. Hii ni kwa sababu anampa Mikidadi mashauri mema. Licha ya mamake, kuna wahusika wengi ambao ni wasaidizi wa Mikidadi kama vile: sultani, waziri katika wakati tofauti wanamsaidia Mikidadi katika kupata mali aliyotumia kumwoa Mayasa.

Mikidadi anapotoka kutafuta mali ili amwaoe Mayasa anatoka peke yake. Vitendo vya kunyang'anya watu mali anafanya peke yake kwa hivyo inaonekana kisa hiki hakina mtumwa dhahiri.

Kati ya ubeti 582 hadi 639, kuna kisa cha kusilimishwa kwa Mikidadi na Mayasa na Ali, baada ya kisa cha Mayasa kushinikiza anataka taji alilokuwa amevalia Fatuma akiwa na mumewe Ali. Katika kisa hiki, Mikidadi na Mayasa wanachukua dhima ya nguli. Wanalitaka taji alilovaa Fatuma. Fatuma ndiye mpokezi, kwani ana kile kinachotafutwa na nguli. Kwa kuwa Ali ni shujaa ambaye Mikidadi hawezi kushinda ili aitwae taji, Ali ni mpinzani. Kinachogombewa hapa ni taji, hivyo taji ni kifaa.

Kwa upande mwingine, Ali na Fatuma kwa wakati huo huo ni wapinzani, kwani walimtaka Mikidadi, ambaye ni mpinzani sasa, asilimu. Kama sivyo, Mikidadi angeuliwa na Ali. Ubeti wa 605 na 606 unadhihirisha uhalisi huu. Tunasimuliwa katika ubeti 605 kuwa Mikidadi waliingia vitani na Ali na kuanza kupigana:

Wakisa hayo kunena,
Wakaingia kupigana,
Mikidadi akaona,
Pumzi kupotea

Katika ubeti 606, tunasimuliwa pia Mikidadi alikuwa na wasiwasi mwingi kwa sababu ya Mayasa.

Kawana mera ya pili,
Kapotewa na akili,
Akarudi tashili,
Kwa Mayasa kurejea

Beti hizo mbili zinadhahirisha kuwa Ali hakuwa na haja ya kumuua Mikidadi. Katika ubeti 611, tunasimuliwa kuwa Ali alikuwa mvumilivu na hakupenda kumuua Mikidadi.

Pakasimama ghubari,
Akasihi haidari,
Ali mwingi wa saburi,
Hakupenda kumuua

Kwa hivyo, imani ya Mikidadi na Mayasa, inakuwa kifaa katika kisa hiki. Katika beti 624 na 625, zinaonyesha azma ya Ali. Katika ubeti 624, tunasimuliwa kuwa Ali akimweleza Hamza juu ya ushujaa wa Mikidadi:

Ali akamweleza,
Sikia baba Hamza,
Tangu kale hapo kwanza,
Sioni mtu shujaa

Katika ubeti 625, tunaendelea kusimuliwa jinsi ambavyo Ali angetaka Mikidadi asilimu ili wawe pamoja katika vita vya jihadi kwa sababu ya ushujaa wake.

Na amuye amwambie,
Mimi napenda mtwae,
Asilimu tuwe naye,
Alii akaridhia

Hatimaye, Mikidadi na Mayasa wakasilimu. Huku kusilimu kulimsaidia Mikidadi kwani kama si waislamu, kwa ujanja wa Jabiri, Mikidadi angeuawa na jeshi la Maliki. Malaika Jibrili anatokea na kumwongoza mamake Mikidadi kwa Mtume Mohammed kutaka msaada. Msaada unapatikana kwa kumtuma Hamza na Ali na wanamuokoa Mikidadi.

Kisa hiki pia kinatupa fursa ya kuchunguza wahusika tena upya. Mamake Mikidadi na Mtume Mohammed ni nguli wanaotafuta uhuru wa Mikidadi. Mikidadi ni kifaa, anatafutwa na mamake na Mtume Mohammed. Maliki ni mpinzani wao. Hamza na Ali ni watumwa, wanamsaidia Mtume Mohammed na mamake Mikidadi kumtafuta Mikidadi. Aidha jeshi la Maliki ni watumwa wa Maliki. Kwa upande wa Maliki, Mayasa ni kifaa Mikidadi ni mpinzani wao, ndiposa wanadhamiria kumuua. Kwa upande wa

mamake Mikidadi na Mtume Mohammed ni wasaidizi wa Mikidadi ili asiuliwe na jeshi la Maliki ni mpokezi.

Rimmon – Kenan (2002), baaada ya kujadili mawazo ya Greimas pia anapiga hatua na kujadili mawazo ya Ewen (1971 na 1980), katika harakati za kutoa mwanga katika mada ya mhusika. Rimmon – Kenan anaelezo kuwa, uainishaji wa mhusika wa Forster (1927) wa mhusika bapa na mviringo haufai. Anapendekeza mtazamo wa Ewen kuwa, mhusika achunguzwe kwa kufululiza (continuum) badala ya kategoria tenge kama za Forster. Kwa hivyo anaonyesha kufululizwa huko, kama kuna kujumlisha: utata, ukuaji na upenyaji katika ndani ya maisha ya mhusika. Tutachunguza kufululiza huku, hapa.

Rimmon – Kenan (2002) anaeleza katika safu ya utata tunapata wahusika wanajengwa kupitia hulka moja au kupitia hulka moja kuu na nyingine chache ndogo ndogo. Kwa hivyo, wahusika wasiobadilika sana wanapatikana katika kategoria hii katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Mhusika Maliki anaakisi maelezo haya. Hata baada ya kusikia Mayasa ameposwa na Mikidadi anafanya njama na babake kumwoa Mayasa, pasi na Mayasa kuridhia. Mikidadi anaporejea na kupigana na kuua jeshi lake Maliki na kumtwaa Mayasa, hatosheki tena na wanapanga mpango wa kutaka kumwoa Mayasa tena, lakini wakati huu kwa kumuua Mikidadi mpaka Hamza na Ali wanatumwa kumwokoza Mikidadi. Hatimaye Maliki anauawa na Mikidadi. Katika ubeti 751 na 752 tunasimuliwa kifo cha Maliki mikononi mwa Mikidadi:

Akampa Mikidadi,
Na maguuni kuyudi
Kumtinda asibuhi
Kamkata saa moja

Kamtinda binafusi
Kamkata yake rasi,
Roho yake kwa upesi
Mstuni ikenda tiwao

Pili, Rimmon – Kenan (2002), anaeleza kuwa kinyume cha wahusika waliojengwa kwa hulka moja ambao ni sahili na wanaainishwa kama wahusika wadogo; ni wahusika ambao wamejengeka kikamilifu, kwa hivyo ukuaji wao ni wa kina. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, wahusika wakuu Mikidadi na Mayasa wanaafiki maelezo haya.

Kwanza, Mikidadi kijana anayedharauliwa kama mchungu mifugo anaibuka kuwa shujaa kwa kuwashida watu wote na kumshida Mayasa vitani, hivyo Mayasa kumteuwa aitwe mumewe. Aidha, Mikidadi mkata anapotoka kwao anarudi mkwasi baada ya kutafuta mali. Hali kadhalika Mikidadi shujaa anakamatwa na jeshi la Maliki nusura afe mikononi mwa Maliki kama si msaada kutoka kwa Mtume Mohammed.

Pili, Mayasa shujaa aliyepigana na wengi na kuwashinda anabadilika kwa kuozwa Maliki shingo upande badala ya kupigana naye. Hata mara ya pili, Mikidadi anapochukuliwa

mateka, Mayasa hamsaidii bali tunampata katika hali ya unyonge, amekaa na Maliki kustarehe ilhali mumewe mteule anakaribia hatari ya mauti katika ubeti 746:

Kajitia Mikidadi,
Pasipo kubisha hodi,
Amwone meraghidi
Na mkewe amekaa

Kwa kweli, huyu siye Mayasa wa mwanzo katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, amebadilika sana. Hivyo amedhihirisha, mhusika aliyekuwa kikamilifu.

Tatu, Rimmon – Kenan (2002) anajadili kuhusu upenyaji katika undani wa maisha ya mhusika. Katika mfululizo huu, saikolojia ya mhusika inachunguzwa. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, tunaweza kuchunguza, maisha ya Mikidadi na fikira zake. Undani huo unatupa sababu za Mikidadi kutenda alivyotenda. Babake aliyekuwa tajiri hakumrithisha chochote, kwa hivyo kumwachia ufukara unaomtia mbioni kutafuta mali ili afunge ndoa, hivyo kuchochea ushujaa wake.

Rimmon–Kenan (2002), anaeleza kuwa kutokuweco kwa mielekeo inayoonekana ni mtafaruku katika nadharia ya mhusika ambao ni mwaliko wa utafiti zaidi katika kipengee hiki cha naratolojia.

2.4.2 Uhusika

Baada ya kuchunguza mhusika katika sehemu iliyotangulia ni bora kugeukia uhusika. Tofauti na mhusika, uhusika umeelezwa kwa uzuri katika naratolojia.

Uhusika ni kipengee kinachotokana na matini kwa hivyo ni rahisi kuchunguzwa. Rimmon – Kenan (2002), anaeleza uhusika kama sehemu ya hadithi, inayoelezwa kupitia sifa za mhusika. Kwa hivyo, kwa mujibu wa Rimmon – Kenan, uhusika ni hulka au sifa anayowakilisha mhusika. Rimmon- Kenan (2002), anaendelea kueleza kuwa, arki yoyote katika matini inaweza kuakisi uhusika. Hii ina maana kuwa, uhusika unaweza kudadavuliwa kupitia arki nyingi katika matini.

Kwa mujibu wa Rimmon – Kenan (2002), kuna viakisi viwili vya uhusika katika matini. Viakisi vinaweza kuwa dhahiri au visiwe dhahiri. Tutavichunguza hapa.

2.4.2.1 Viakisi Dhahiri vya Uhusika katika Matini

Kiakisi cha aina hii hutaja hulka kwa kutumia vivumishi. Yaani msimulizi katika matini yake anataja hulka katika kazi yake. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, msimulizi ametaja hulka zifuatazo katika matini ya *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Katika ubeti 2, anajitaja kama asiye na makini. Ubeti wa 15, Mikidadi ni mnyonge. Ubeti wa 19, Mayasa ni mzuri kwa urembo wake uliokithiri. Ubeti wa 33, Mayasa ana maringo kwa ushujaa wake. Ubeti wa 123, Mikidadi ni yatima asiye na lolote. Ubeti wa 177, jinsi afiriti ametajwa. Ubeti wa 29, Luhani anatajwa kuwa mfalme.

Kutokana na mifano hiyo hapo juu, tunahitimisha kuwa uhusika unaodhihirika katika matini umetumika katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

2.4.2.2 Viashirii vya Uhusika Visivyodhahiri

Rimmon – Kenan (2002,) anaeleza kuwa viashirii visivyokuwa dhahiri havihitaji hulka bali huonyesha tu. Anaendelea na kujadili viashirii hivi kama: matendo, usemi, muonekano wa nje, mazingira na mfananisho. Katika sehemu hii tutachunguza viashirii hivi.

2.4.2.2.1 Matendo

Rimmon – Kenan (2002), anaeleza kuwa uhusika unaweza kudokezwa kwa matendo ya mazoea au ya mara moja. Matendo haya yanaweza kuwa yaliyotendeka, yasiyotendeka au yanayofikiriwa. Kwa kurejelea maelezo haya, katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, tukirejelea Mikidadi, kwa jamii ni shujaa anayepigana mara nyingi na kushinda. Lakini pia ni mwenye uoga, aliogopa kunyakua taji la Fatuma kwa kohofia mumewe.

Pia, Mikidadi ni mwenye matumaini, licha ya kutokuwa na mali aliazimia kumuoa Mayasa hata nasaha ya mamake haikumtamausha.

Kwa upande wake Mayasa, ni shujaa, alipigana kishujaa na waposi wake hadi aliposhindwa na Mikidadi. Mayasa ni mnyonge, anaacha aolewe na Maliki licha ya kuwa hakumpenda. Pia, anatamaa, alitamani taji la Fatuma licha ya kuwa lilikuwa na mwenyewe.

Kitendo cha Ali kutomuua Mikidadi kinatupa fursa ya kupata uhusika kupitia tendo lilikosa kutendeka. Kwa hivyo, Ali ni mwenye utu mwingi wa huruma. Kwa sababu Mikidadi alichokoza na Ali hakumuua. Ali angemuua Mikidadi haingekuwa makosa.

2.4.2.2.2 Usemi

Rimon – Kenan (2002), ameeleza kuwa usemi wa mhusika katika mazungumzo au mjadala akilini (uwasilishaji wa mawazo) unaakisi uhusika. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, umeonyesha asili mia kubwa ya daigesia, yaani hatuoni usimulizi wa wahusika moja kwa moja bali tunapata kupitia maelezo ya mhusika. Hata hivyo, fomula ya ufunguzi inatupa fursa ya kumchunguza msimulizi kwa kuwa ndiye sauti yake tunaisikia kwa uhakika.

Kutokana na fomula hizi tunapata msimulizi ana hulka zifuatazo. Muumini kwa sababu anatanguliza utenzi kwa sala. Ni mnyenyekevu, katika ubeti 2, anakiri hana ujuzi wa kutunga utenzi :

Bismillahi mbuyaza

Awali ya kujifunza

sijui taufawaza

Au vitanichachia (ubeti 1)

Kwa kuwa sina makini

Sina fahamu moyoni

Kwa dunia kuwa duni

Tangu sasa nawambia (ubeti 2)

Ni msimulizi hodari, kwa sababu katika ubeti 777, amejitapa baada ya kusimulia kisa cha Mikidadi na Mayasa.

Kisa utendi wa vita,
Simulia yaliopita
Hijazi yenye matata,
Jamaa nimewambia (ubeti 777).

2.4.2.2.3 Muonekano wa nje

Rimmon – Kenan (2002), anaeleza kuwa muonekano wa nje umetumiwa kukisia uhusika. Anatoa mfano wa, mhusika mwenye macho ya hudhurungi yanayoonyesha huzuni. Kiashirii hiki kinadhihirika vyema katika riwaya, kwani katika ushairi, msimulizi hana mwanda mkubwa wa kimaelezo kama hayo bali hutoa tu matendo muhimu katika hadithi yake. Licha ya hayo, *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* umeonyesha arki hii katika ubeti 18 hadi 21, katika kuelezea uzuri wa Mayasa, tunasimuliwa katika ubeti wa 19, kuwa;

Mayasa ali mzuri
Na weupe wa fakhari,
Na uso wake duwari
Kusema na ushujaa (ubeti 19)

Uzuriwe na jamali
Habari zikenda mbali
Wakasikia kabaili
Na sifa zikatangaa (ubeti 21)

Maelezo ya ubeti huu tunapata kuwa Mayasa ni mrembo, ndiposa Mikidadi akampigania kwa udi na ambari.

2.4.2.2.4 Mazingira

Rimmon – Kenan (2002) ameeleza kuwa mazingira ya kimaumbile kama vyumba, barabara, mji na msitu na mazingira ya kibinadamu kama aila, tabaka na uhusiano aghalabu hutumika kuelezea uhusika.

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, Mikidadi ni fukara na Mayasa ni tajiri. Luhani ni mfalme, aidha kuna waziri katika ubeti wa 360.

Urathi wa baba yake

Mikidadi asishike

Hakuwa hata na mke

Kwa unyonge kumwingia (ubeti 15)

Ubeti huu unaelezea mazingira yaliyosababisha ufukara wa Mikidadi.

2.4.2.2.5 Mfananisho

Rimon – Kenan (2002), anaeleza kuwa mfananisho unaweza kuelezea uhusika. Katika mfananisho huu anajadili sitiari. Ameonyesha kuna mfananisho wa majina na mazingira. Haya yote tuliweza kubaini ni matumizi ya mbinu ya majazi. Kwa hivyo majazi, tashbihi na sitiari ni mbinu tatu za mfananisho anaokusudia Rimmon–Kenan. Kwa mfano Mikidadi kufananishwa na simba katika mshororo wa nne ubeti ufuatao :

Khabarize Mikidadi

Zikaenea biladi

Kuwa wadi murtadi

Kama simba alokaa (ubeti 282)

Kwa kuwa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni tafsiri kutoka kiarabu, majazi yake si dhahiri katika Kiswahili. Hata hivyo, sitiari itasadifu.

Sitiari inayojitokeza katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni pamoja na Ali kuitwa Haidari (simba) katika Ubeti 621.

Simuue Haidari

Zidi moyo kusubiri

Akatoa na shairi

La kumsifu Alia

2.5 WAKATI WA USIMULIZI

Katika kipengele hiki kinaeleza usimulizi na matukio katika hadithi. Matukio yanaweza kusimuliwa katika usimulizi baadaye, kabla au sambamba.

2.5.1 Usimulizi baadaye

Katika usimulizi huu, msimulizi anasimulia kilichotendeka wakati uliopita wakati huu kihadithi. Usimulizi baadaye ndio unatamalaki usimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kutoka ubeti 12 hadi ubeti 777. Katika ubeti 777, msimulizi anadokeza kiashirii

cha usimulizi baadaye, kwa maneno yake anaposema kwamba amesimulia utendi wa kisa cha vita kilichopita.

Kisa utendi wa vita,

Simulia yalopita

Hijazi yenye matata,

Jamaa nimewambia (ubeti 777).

Matumizi ya viambishi ‘lo’ yaani ‘li’ na ‘me’ katika mshororo wa pili na wa nne mtawalia itafasiriwa kama hadithi yenyewe ni ya zama japo usimulizi wenyewe ndio umekamilika hivi punde, ndiposa kiambishi ‘me’ kikatumiwa katika mshororo wa mwisho ubeti huo wa 777.

Katika ubeti 242, msimulizi anasimulia akitumia kiambishi cha nafsi ya tatu na wakati usiodhihirika ‘a’:

Akaketi siku tatu,

Na mali yake na vitu

Siku yane wene watu

Wangi wakipita ndia.

Matumizi ya “a” ya wakati usiodhihirika yameshamiri utenzini. Hata hivyo, ubeti 13, msimulizi anasimulia;

Suwedi ali tajiri

Ali na mali kathiri,

Ali mwingi wa safari

Mali akajitumia.

Matumizi ya awali katika hadithi ya kiambishili “li” yanaifanya “a” isiyodhihirika kufasirika katika wakati ujao, hivyo kutoa athari za hali isiyodhihirika. Kwa kutumika kama katika vitenzi vikuu vinavyotumiwa na visaidizi vinavyobeba hali huku kitenzi kisaidizi kikibeba njeo. Kwa sababu za kukisaidia basi vitenzi visaidizi vinadondolewa na kubakisha tu, vikuu. Ndiyo maana “a” isiyodhihirika kutawala kimatumizi. Hata hivyo, utenzi kwa ujumla uko katika njeo iliyopita. Hivyo, kuleta dhana ya usimulizi baadaye.

2.5.2 Usimulizi Kabla

Katika usimulizi huu, msimulizi husimulia matukio yatakayotokea siku zinazokuja. Usimulizi huu huchukua mkondo wa kubashiri au ndoto.

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, huu usimulizi unapatikani kwa kiasi kidogo sana. Baada ya vita vya Mikidadi na Jeshi la Maliki, Hamza alimwambia Ali angetaka Mikidadi asilimu kwa sababu ya siku ya kيامa. Ilimhitaji Mikidadi kumkubali Mtume Mohammed kama Mtume wa Mungu wa pekee ili kuingia paradiso baada ya kifo. Ubeti wa 624 unadhahirisha haya.

Na amuye amwambie

Mimi napenda mtwae

Asilimu tuwe naye

Alii akaridhia

Aidha kuna mfano mwingine wa usimulizi kabla wakati ambapo Ali alimwambia Mikidadi kulikuwa na jambo alilotaka kumfunza. Ali akamwambia Mikidadi arudie ombi

ambalo angekuwa akilinena wakati wa shida na ndilo lingemwepusha na shida hizo na kumfikisha paradiso. Ubeti wa 625 unadhihirisha haya:

Neno hilo unenapo

Ulimi utamkapo

Makazi yako ni pepo

Ndimmo wendamo kukaa.

Mfano mufti wa matumizi ya arki hii ya usimulizi kabla unapatikana katika *Utenzi wa Qiyama*, ambao unasimulia matukio yatakayotokea wakati dunia itakapoisha.

2.5.3 Usimulizi Sambamba

Huu ni usimulizi unaoenda sawa na jinsi matukio yanavyotokea. Katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, usimulizi huu haupatikani sana, kwa sababu kama tulivyokwisha eleza, utenzi ulitokana na usuli wa kitabuni. Licha ya hayo, matini ya kufungua na kutamatisha kwa utenzi zinaweza kufasiriwa kuwa zinatendeka anaposimulia. Hii ni kwa sababu asili ya tenzi hizi ni fasihi simulizi ambayo baadaye ilipata kuandikwa.

2.6 Utegemefu wa Msimulizi

Kwa mujibu wa Rimmon- Kenan (2002), msimulizi mtegemefu anasimulia hadithi kwa njia ya kuaminika kama ukweli wa kibunilizi. Vinginevyo, atakuwa msimulizi asiye mtegemefu.

Tunaafikiana na Rimmon-Kenan (2002) kuwa kunaweza kuwa na viwango tofauti vya utegemefu. Hata hivyo, swala hilo hatutalishughulikia hapa. Ijapokuwa tunaafikiana na dalili alizotoa zinazoashiria kutokuwa mtegemefu kama: msimulizi kuwa na ujuzi haba kuhusu hadithi, kujihusisha katika hadithi na tatizo la kutathmini maadili.

Katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, msimulizi ameonyesha kuwa ana ujuzi wa kutosha kuhusu hadithi yake japo inapatikana kitabuni. Kwa upande wa kujihusisha, msimulizi anajitokeza kama asiyejikusisha katika hadithi anayoisimulia.

Aidha, tathmini yake ya maadili ni ya kiwango cha hoja ikitiliwa maanani kuwa ni utenzi uliokita katika imani za kidini. Hivyo, tathmini yake haina pingamizi. Kwa kuzingatia hayo yote *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unadhihirisha msimulizi mtegemefu kulingana na vigezo vya Rimmon-Kenan (2002). Anaifahamu hadithi zima na kuisimulia kwa kina kana kwamba alishiriki katika hadithi. Hivyo ana ujuzi wa kutosha na anaweza tegemewa. Hali kadhalika tathmini yake ya maadili ameiweka wazi ya dini ya kiislamu.

2.7 Hadhi ya Msimulizi

Hadhi ya msimulizi ni dhana inayorejelea mbinu ya uwasilishaji wa usimulizi. Mbinu hii inaweza kuwa mbinu ya kidaigesia au kimimesia. Kwa mujibu wa Rimmon-Kenan (2002) uwasilishaji wa mimesia unahusisha wahusika (waigizaji) wakiwa katika jukwaa wakiigiza kama katika tamthilia au drama. Huzungumza na kufanya ishara sawia na watu wafanyavyo katika maisha halisi. Usimulizi wa kidaigesia nao, unahusisha hadithi kuwasilishwa kupitia maneno. Hivi kwamba vitendo, ishara huelezewa tu, haviigizwi.

Utendi wa Mikidadi na Mayasa, unadhihirisha zaidi usimulizi wa kidaigesia kuliko ilivyo kimimesia.

Kwa mfano katika ubeti 354 na 358 tunasimuliwa juu ya Sultani alivyomwita waziri wake na maelezo ya sifa za waziri huyu zinafafanuliwa na msimulizi na jinsi waziri alivyopokea maneno ya Sultani.

Sultani kakariri

Kamwita wake waziri

Naye ni mtu basiri

Usemi na ushujaa. (ubeti 354)

Waziri akabaini

Marahaba Sultani

Takuletea mjini

Kaondoka kamwendea (ubeti 358)

Ubeti huu unaweza kuwasilishwa kivitendo, hata hivyo, msimulizi amechagua mbinu ya kuhadithia bila kuhusisha kuonyesha vitendo wala usemi. Hivyo kuendelea kudumisha daigesia kama mbinu yake ya kutuwasilishia *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

Hata hivyo, wananaratolojia wanahoji ikiwa usemi unaweza kuwa daigesia au mimesia pekee. Mjadala huu unaonyesha kupoteza mashiko yake kwani msimulizi amejizatiti na kuwasilisha *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kidaigesia.

2.8 Hitimisho

Katika sura hii tulitalii kipengee cha wanaratolojia cha usimulizi. Katika kipengee cha sampuli za wahusika, tulipata kuwa, msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni msimulizi nje. Tukirejelea viwango vya usimulizi, inadhihirika kuwa, usimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni wa daraja ya kwanza kwa kuwa hadithi yenyewe haijaegemezwa vijihadithi vingine. Katika kipengee cha uhusika wa msimulizi katika hadithi ilibainika kuwa msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni msimulizi asiyejikusisha na hadithi anayosimulia.

Katika sehemu ya uhusika na mhusika, tumechunguza uhusika na kupata kuwa ni sifa zinazohusishwa na mhusika. Uhusika unaweza kuwasilishwa waziwazi na pia uwasilishi usiodhahiri kupitia viashirii. Aidha, katika sehemu hii ya uhusika tumeshughulikia uhusika kwa kurejelea viashirii visivyokuwa dhahiri. Tumechunguza viashirii vifuatavyo: vitendo, usemi na mawazo, muonekano wa nje, mazingira na mfananisho.

Katika sehemu ya mhusika tumeshughulikia mhusika kama kipengele cha naratolojia. Tumechunguza mhusika kutegemea mawazo ya Greimas hali kadhalika mawazo ya Ewen.

Kwa upande mwingine tumechunguza mhusika licha ya kupuuzwa kwa kipengee hiki na wahakiki wa kisasa, tumechunguza kupitia mtazamo wa wanaratolojia wakongwe (kirasimu) wa Griemas na Ewen. Jambo ambalo limetufanya kugundua kuwa ni eneo

linalohitaji kufanyiwa uchunguzi na utafiti wa dhati kama vile walivyofanyia vipengee vingine.

Uchunguzi pia umedhihirisha kuwa kuchunguza mhusika na uhusika katika mikitadha tofauti ya hadithi na matini yanazindisha utata katika ufafanuzi wa kipengee cha mhusika. Ingalikuwa bora kama dhana hizi zingejumuishwa katika mkutadha mmoja. Maoni yetu ni kuwa utafiti zaidi katika kipengee cha mhusika ufanywe na mhusika na uhusika. Vipengee hivi vioanishwe ili kusahalisha uchunguzi na kuondoa utata tuliokwisha eleza.

Kwa upande wa wakati wa usimulizi tulipata kuwa, usimulizi baadaye ndio umetumika zaidi. Usimulizi kabla umejitokeza kidogo sana. Kwa upande wa utegemefu wa msimulizi, msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni mtegemefu kwa kufuata kaida za kinaratolojia. Hatimaye, hadhi ya msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni ya kidaigesia.

SURA YA TATU

MPANGILIO WA MATUKIO

3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tutachunguza mpangilio wa matukio katika mfuatano wa wakati, uhusiano katika matukio na idadi marudio. Kisha tutafafanua vipengele hivi na kuchunguza kama vimetumika katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

3.1 Mpangilio wa Matukio katika Mfuatano wa Wakati

Matukio yanaweza kusimuliwa katika mfuatano wa kiwakati au kwa kutofuatana au kufungamana nao kama ilivyoelezewa hapo awali. Ikiwa yatasimuliwa kiwakati, msuko na hadithi huwa na mpangilio sawa.

Matukio yanaweza kusimuliwa bila kuzingatia kaida za mfuatano wa kiwakati. Katika hali panapotokeza mfuatano wa ki-anakroni, mfuatano huu una sifa nne:

Mpangilio wa matukio ki-analepsia, ki-prolepsia, masafa na mwanda. Tutatalii sifa hizi katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* katika usimulizi wake.

3.1.1 Analepsia

Rimmon–Kenan (2002), anaeleza kuwa analepsia ni usimulizi wa kurejelea matukio yaliyopita. Ni usimulizi wa tukio la hadithi wakati matukio ya baadaye yamekwisha simuliwa. Ni mbinu inayotoa habari za kale kuhusu mhusika, hadithi au tukio lililotajwa katika matini.

Mtunzi hutumia mbinu rejeshi ili kutupa msingi au usuli wa hali ya mhusika kwa kuyamulika maisha yake ya kabla, kutubainishia misukumo ya mhusika na tatu kuuweka msingi wa kuendeleza dhamira na maudhui ya kazi inayohusika.

Mbinu hii inatumika sana katika riwaya, vivyo hivyo inatumika katika tendi. Mbinu hii ya analepsia imejitokeza katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

Tunarejeshwa nyuma kuelezewa kwa nini Mikidadi ni fakiri. Mtunzi anasimulia maisha ya Suwedi babake Mikidadi na safari nyingi zilizomfilisisha na ndivyo tunaona Mikidadi sasa hivi hana mali kwa sababu hakurithishwa chochote na babake. Ubeti unaofuata unathibitisha matumizi ya analepsia.

Suwedi Ali tajiri

Ali na mali kathiri

Ali mwingi wa safari

Mali kajitumia (ubeti13)

Urathi wa baba yake

Mikidadi asishike

Hakuwa hata na mke

Kwa unyonge kumwingia (ubeti 15)

Aidha msimulizi anasimulia jinsi Mikidadi alienda vitani ili kutafuta mali ya kumposa Mayasa kuanzia ubeti wa 167 hadi 462. Msimulizi anasimulia jinsi Mikidadi alivyopigana kijasiri kama simba na sifa zake zikaenea kote.

Khabarize Mikidadi

zikaenea biladi

Kuwa wadi murtadi

Kama simba alokaa (ubeti 282)

Mifano mingine ni masimulizi ya njama iliyopangwa na kina Maliki kumuua Mikidadi lakini aliokolewa na malaika Jibrili na Mikaili walioandamana na Tamima, mamake Mikidadi kwa Mtume Mohammed ili Mikidadi apate kuokolewa (ubeti 688-718).

Hiyo ni baadhi ya mifano ya matumizi ya analepsia kama arki moja ya simulizi bunilizi katika utendi wa kale wa Kiswahili kama inavyotumika katika riwaya.

3.1.2 Prolepsia

Pia inaitwa mbinu elekezi au kiona-mbele. Rimmon-Kenan (2002) anaeleza kuwa ni usimulizi uelekezi wa tukio la hadithi la baadaye kabla ya kutokea kwake. Msimulizi anatuangazia matukio ambayo hayajatokea.

Prolepsia inapatikana sana katika kazi zenye mielekeo ya kinjozi au kitabiri. Mbinu hii imetumika katika utendi wa *Quyama*, utungo unaosimulia maisha wakati wa siku ya mwisho au kiama katika misingi ya dini ya kiislamu. Rimmon-Kenan (2002), anasema

kuwa mbinu hii inatofautishwa na udokezaji wa tukio la wakati ujao. Ni mbinu ambayo si maarufu kama ilivyo analepsia.

Mbinu ya prolepsia imetumika katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* lakini kwa kiasi kidogo sana. Kwa mfano baada ya vita vya Mikidadi na jeshi la Maliki, Hamza alimwambia Ali kuwa angetaka Mikidadi asilimu. Hamza walikuwa wanazungumzia sifa za kishujaa na Ali na wakamtaka ajiandae kwa siku ya kiyama kwa kumkubali Mtume Mohammed kama Mtume wa Mungu wa pekee. Haya ni maisha ya baadaye ambayo ni kama utabiri.

Kisha Ali akamwambia Mikidadi kuna jambo alikuwa anataka kumfunza. Akamwambia arudie ombi ambalo angekuwa akilina wakati wa shida na ndilo lingemfikisha paradiso kwa kumtambua Mtume Mohammed. Ali alikariri ombi lile naye Mikidadi akanena nyumaye kwa kusudi la Mikidadi kujiandaa kuingia paradiso.

Ali akaradidi

Isma ya Mikidadi

Inda kalima wahidi

Nitakaya kukuambia (ubeti 626)

Neno hilo unenapo

Ulimi , utamkapo

Makazi yako ni pepo

Ndimu wendamo kukaa (ubeti 625)

Katika beti hizo mbili 626 na 625 zinadhihirisha matumizi ya prolepsia hasa katika matumizi ya wakati ujao kwa kutumia kiambishi cha wakati ujao [ta] kama alivyoelezea Rimmon- Kenan (2002).

Manfred (2006), ameiita mbinu hii Kiona-mbele ambayo ni maono ya mhusika kuhusu tukio la baadaye katika hadithi kama vile Mikidadi anavyoarifiwa kuwa akinena maneno fulani shida zake zitaondolewa na pia hali ya kuingia paradiso ambayo ni ya baadaye au utabiri wa siku ya kiamaa.

3.1.3 Mwanda

Guillemette na Levesque (2006) wanaeleza kuwa mwanda (extent) ni muda ambao anakroni inachukua katika hadithi. Anakroni ni hali ikitokea kwamba matukio yanasimuliwa bila ya uzingatiaji wa kaida ya mfuatano wa kiwakati. Mfuatano huu una sifa ya kurejelea nyuma au kuelezea mbele. Mwanda huu unaweza kuwa wa kiprolepsia au kianalepsia ambao unaweza kuwa mrefu au mfupi. Kwingi mwanda wa kianalepsia ndio unaotumika au kupatikana sana.

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* mwanda umetumika kwa wingi kwa kianalepsia kuliko kiprolepsia. Msimulizi anasimulia hadithi kuanzia ubeti wa 13-625, kisha kuanzia ubeti 698-778. Anasimulia kuhusu maisha ya Suwedi, Turadi, vita kati ya Mikidadi na Mayasa ambavyo vimechukua mwanda mrefu katika hadithi baadhi ya matukio mengine.

Msimulizi ametumia muda mrefu kwa kusimulia matukio ya awali tofauti na ya kutokea baadaye. Mwanda wa kiprolepsia uliotumika ni mfupi sana kuanzia ubeti 626-697. Inayoelezewa ni matukio yanayotarajiwa kufanyika kwa mfano kwenda paradiso na matatizo kusuluhishwa baadaye baada ya kunena maneno fulani Mikidadi aliyofunzwa na Ali.

3.1.4 Masafa

Masafa ni kipindi ambacho anakroni inachukua katika hadithi. Kulingana na Rimmon-Kenan (2002), analepsia na prolepsia zinaweza kuchukua kipindi kilicho zaidi ya hadithi ya kwanza, masafa hayo ni ya nje. Pia zinaweza kuchukua kipindi kabla ya hadithi ya kwanza lakini zikaja baadaye kabla ya wakati wake katika hadithi hiyo moja hivyo ni masafa ya ndani. Masafa kulingana na maelezo ya Rimmon-Kenan (2002), basi yanaweza kuwa ya nje au ndani hivyo kuwa masafa mchanganyiko au mseto.

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* masafa yametumika kwa vile utendi unaanza kwa msimulizi kusimulia yaliyo nje ya hadithi kama vile kumtukuza Mungu, Mtume Mohammed na kuomba asimulie hadithi hii.

Anaanza kusimulia hadithi kuanzia ubeti wa 13. Hivyo anakroni (analepsia) inajitokeza baada ya hadithi kuanza kwa kuturejesha nyuma juu ya maisha ya Suwedi babake Mikidadi alivyokuwa tajiri kisha akawa fukara kwa sababu ya safiri nyingi alizosafiri.

Suwedi ali tajiri

Ali na mali kathiri

Ali mwingi wa safari

Mali akajitumia (Ubeti 13)

Kisha msimulizi anaendelea kutusimulia juu ya vijana hawa wawili katika shughuli zao za kutaka kuoana na vita vingi vilivyohusika. Hali kadhalika katika beti 625-697 msimulizi anatueleza yatakayotokea (prolepsia) ya kwamba Mikidadi akisilimu na kumtukuza Mungu na Mtume Mohammed ataingia paradiso na kisha baadaye anaendelea na hadithi jinsi Mikidadi na Ali waliendelea kupigana jihad. Haya ni masafa ya nje. Ni wazi kwamba msimulizi ametumia masafa mseto katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

3.2 Muda katika Usimulizi

Swali tunalojiuliza ni tukio limechukua kipindi kirefu au kifupi katika usimulizi wake na kwenye matini. Genette (1972), anaeleza kuwa wakati katika usimulizi ni vipi hadithi imewasilishwa kufuatia usimulizi mzima na matokeo yake.

Dhana ya muda hurejelea uhusiano katika hadithi wa tukio lenyewe na wakati unaotumika kuwasilisha au kusimulia tukio hilo kwenye matini. Rimmon-Kenan (2002), anaeleza kuwa muda au wakati-usimulizi hushughulikia uhusiano kati ya usimulizi na hadithi. Anaendelea kueleza kuwa wakati-hadithi katika usimulizi ni kipimo cha kasi katika usimulizi ambao ni matokeo ya kugawa wakati wa hadithi na urefu wa matini. Ameorodhesha na kueleza aina nne za wakati hadithi katika usimulizi; muhtasari,

udondoshi, uendelezaji na mtuo. Elementi hizi tutazichunguza zilivyotumika katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

3.2.1 Muhtasari

Hii ina maana kuwa matukio mengine katika hadithi hufupishwa na kuchukua muda mfupi sana kuliko inavyostahili kusimulia matukio haya. Rimmon-Kenan (2002), anaeleza kuwa muhtasari katika wakati ni kasi ya usimulizi inapoharakishwa kwa kubana matini ya kipindi cha hadithi katika kauli fupi za matukio makuu.

Matumizi ya muhtasari yanapatikana katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, baada ya Mikidadi kupigana vita vikali na Mayasa na kukubaliwa kumwoa, aliomba apewe miezi mitatu akatafute mali ya kumposa Mayasa. Katika matini miezi hii mitatu imeelezea baadhi ya matukio machache tu alivyopigana kujipatia mali. Muda huu umeelezewa katika beti 165-697. Muda aliyotumia umebanwa katika masimulizi kwa kutumia beti chache kulingana na matukio yote yaliyotendeka katika muda wa miezi mitatu.

Mikidadi mwana kwetu

Wenenda tafuta vitu

Muda wa myezi mitatu

Uwe hapa nakwambia

Myezi mitatu ikisa

Akija mtu kuposa

Nitamwoza Mayasa

Mikidadi karidhia

Mikidadi alipoanza safari yake na mtumishi mmoja tunaalezewa siku ya nane wanajipata hawana maji na chakula ishara ya kukosa mahitaji ya kimsingi na ambapo siku hizo zingine saba walikuwa na matatizo lakini yanaalezewa kwa siku moja tu waliyoyapitia. Katika ubeti 169 na 171 msimulizi anaelezea matukio ya siku nane.

Siku ya nane kipata

Chakula hapana hata

Maji hayapati kata

Hayo yaliyosalia

Mikidadi atoshele

Hawezi kwenenda mbele

Kwa kiu imzidile

Mtumwawe kamwambia

Safari ya Mikidadi ya kurudi baada ya kunyakua mali imeelezwa kwa ubeti mmoja tu. Anapofika anapata habari kuwa mjini kulikuwa na harusi; kama ilivyo katika beti hizi 487 na 489. Hivi ni kumaanisha kwamba safari yake ya kurudi imebanwa na kusimuliwa kwa ubeti mmoja tu.

Mikidadi kenda zake
Jamii na mali zake
Karibu kupata kwake
Khabari akasikia

Akasikia sahihi
Muyini kuna nikahi
Maliki bin Riyahi
Mayasa ataka oa

3.2.2 Udondoshi

Dhana hii hurejelea pale ambapo maelezo fulani yameachwa katika matini fulani. Wamitila (2003), anaendelea kueleza kuwa kuna mwanda nunge wa kimatini ili hali hadithi yenyewe ina wakati fulani. Hivyo basi wakati-hadithi na wakati-matini huwa tofauti. Kwa mfano, maelezo ya tukio fulani au mhusika fulani hayajatolewa kwa muda fulani.

Utendi wa Mikidadi na Mayasa unaakisi elementi hii ya usimulizi katika beti 665-697. Hapa ni mwanda ambao Mikidadi alienda kutafuta mali ya kumwoa Mayasa, msimulizi hajatoa maelezo ya Mayasa alipokuwa akifanya alipokuwa akimngoja Mikidadi.

Mfano mwingine ni safari ya Tamima kwenda Medina kumwona Mtume Mohammed ili wamuokoe Mikidadi kutokana na hila za Maliki. Mungu anamtuma mtume Mikaili

aende aikunje nchi ili Tamima aweze kusafiri haraka. Naye malaika Jibrili alitumwa kwa Mtume Mohammed ili wawe wamejiandaa kumpokea Tamima kama inavyodhihirika katika beti zifuatazo.

Tena Rabi kamtuma

Mikaili shuka hima

Ajuza enda kwa Tumwa

Upesi kusikilia (ubeti 698)

Na nti ikundekunde

Safari yake enende

Pasipate muda punde

Madina akatokea (ubeti 699)

Katika vita vya Mikidadi na Maliki hatujatolewa maelezo kana kwamba Jabiri alihusika katika vita hivi ili kumsaidia Maliki.

3.2.3 Onyesho

Katika onyesho, wakati hadithi na wakati matini huwa sawa kulingana na Rimmon-kenan (2002). Mazungumzo ni njia mojawapo ya kulidhihirisha onyesho. Ni njia ambayo huleta sifa ya uigizaji katika matini yoyote ile. Msimulizi husimulia hadithi kama kwamba wanaohusika wanaigiza mbele ya msomaji (msikilizaji). Rimmon-Kenan anaendelea kueleza kuwa matini ikiwa na dayalojia na maelekezo kwenye jukwaa, usimulizi huo unaonekana kama onyesho kutoka kwa mchezo wa kuigiza na wala si

sehemu ya msimulizi hadithi fulani. Elementi ya onyesho imetumika katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

Kuna mazungumuzo kati ya Jabiri na waposi wa Mayasa kuanzia ubeti (28-35). Msimulizi anatusawiria wahusika kana kwamba wanaigiza yale ambayo wananena. Hali kadhalika tunamwona msimulizi mwenyewe anayaiga maneno yale hasa anapotumia nafsi ya kwanza. Tazama mshororo wa pili hadi wa tatu ametumia ‘tu’ na ‘ni’ katika beti zifuatazo.

Wakamwambia Jabiri

Tujulie *tuna* shauri

Tuna mali akthari

Tujile kutaka ndoa (ubeti28).

Jabiri akawajibu

Nisikizani warabu

Mwanangu ana aibu

Kwa hayo mloniambia (ubeti 30)

Mazungumzo hayo yanatamatishwa na Jabiri anapoondoka kwenda kuongea na Mayasa ubeti 37-40. Msimulizi anasimulia moja kwa moja yale yanayonenwa na wahusika bila kutumia alama za usemi halisi na hivyo kufasiriwa kuwa anayaiga maneno na vitendo ya wahusika Jabiri na Mayasa.

Mwanangu kujile watu
Wangwana wenye vitu
Kusudi wajile kwetu
Ili kutaka kuoā (ubeti 37).

Mume wangu nitakaye
Hapa pangu anijiye
Tupigane mimi naye
Anishindapo taoā (ubeti 39).

Mazungumzo haya yanadhihirisha hali ya kuigiza kwa vile kuna maelezo ya vitendo vinavyotendeka. Kwa mfano tunaelezewa Jabiri akienda na kurudi kuongea na waposi na Mayasa na baadaye anawataja hadharani wote kwa majina waliokuwa wamekuja kumposa Mayasa.

Kuna mazungumzo kati ya Mikidadi na mjombake Turadi na mamake Tamima kuhusu uamuzi wa Mikidadi kupigana na Mayasa ili amuoē. Haya yanathibitishwa katika utendi beti za 30, 81, 82, na 83.

Mjomba nipe farasi
Unazime na libasi
Nimtokee Mayasa
Napenda kumtokea (ubeti 81)

Mjombawe akanena

Hutaweza kupigana

Kwani ungali kijana

Vita havijakuelewa (ubeti 82)

Mifano mingine ya elementi ya onyesho katika simulizi ni mazungumzo kati ya Mikidadi na afriti Shaitani (beti 177-181). Mikidadi anapotafuta maji ya kunywa, Mikidadi na mtumwa wake Khamisi (ubeti 182) kuhusu ukosefu wa maji na kipumziko baada ya kisa cha afriti, Mikidadi na Luhani kuhusu mpango wa Luhani kumuua kijana Kesi mumewe Anasa (ubeti 214-220), Mikidadi akiwauliza Anasa na Kesi wangetaka awafanyie nini ili kuepukana na hukumu ya kifo kutoka kwa Luhani (beti 203-204), Turadi na Jabiri baada ya Mikidadi kurudi kutoka kutafuta mahari (506-501), Mayasa na jeshi la Maliki ili Mayasa kuamua nani angemuoa (beti 563-571) na Ali, Hamza na Mikidadi wakati ambapo Mikidadi alisilimu na kuwa muislamu (ubeti 624-637).

Hiyo ni baadhi ya mifano mingine mingi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ya wakati hadithi wa onyesho.

3.2.4 Mtuu

Rimmon-Kenan (2002), anaeleza kuwa mtuu au uendelezaji ni dhana inayorejelea matukio katika hadithi yakikatizwa ili kuachia nafasi maelezo katika hadithi. Msimulizi anayaangaza mawazo ya mhusika. Sifa hii inajitokeza penye maelezo yanayofungamana na saikolojia.

Arki hii ya wakati imetumika katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Katika fomula ya ufunguzi tunakutana na msimulizi kuanzia ubeti 1-12 akitoa maelezo yasiyohusiana na hadithi. Anaanza kwa kumtukuza Mungu, Mtume Mohammed na kumshukuru Mungu kwa kumpa ujuzi wa kuandika kitabu hiki. Ametumia elementi ya mtuo au uendelezaji kwa vile amekatiza maendelezo ya hadithi kuu.

Kwingine msimulizi ametumia mtuo ni katika (ubeti 203-225), anasimulia kuhusu Anasa na mumewe Kesa. Hawa ni wahusika ambao wako nje ya matini au hadithi kuu na wanasitisha kuendeleza kwa matukio katika hadithi kuhusu wahusika na matukio makuu.

Akawauza wambao

Nambieni mtakao

Kadiri mtamano

Ni mwenye kuwatendea (ubeti 203).

Yule Kesi katongoa

Kamba waweza muua

Ni kheri ukamondoa

Humu katika dunia (ubeti 204).

Usimulizi mtuo unadhihirika pia katika vita vya Mikidadi na afriti (beti 171-181). Masimulizi haya yanakatiza hadithi kuu. Msimulizi ametumia muda kutusawiria mhusika Mayasa kwa kufafanua urembo wake kwa kina katika ubeti 18-21 hivyo kusababisha mtuo katika masimulizi ya hadithi kuu.

Elementi hii imetumiwa katika kutamatisha utendi huu katika ubeti wa 778. Msimulizi anasimulia yanayomhusu mwenyewe kwa kujitambulisha ndiye msimulizi wa hadithi.

Nami mwenye kuradidi

Ismu yangu Saidi

Wa Abdalla Masudi

Jina langu nawambia.

3.3 Idadimarudio/Umara

Rimmon-Kenan (2002), anaeleza kuwa umarudio ni uhusiano baina ya idadi ya mara tukio linavyojitokeza katika hadithi na idadi ya wakati tukio hilo linavyosimuliwa au kutajwa katika matini (uk: 57). Anaendelea kueleza kuwa ingawa kuna marudio ya tukio katika matini, mara nyingi tukio lile linaporudiwa hudhihirisha maana tofauti kwa sababu ya mandhari mapya.

Rimmon-Kenan amesainisha aina tatu za urudio. Aina hizi za idadimarudio ni urudio mara moja, urudio mara nyingi na urudio sikitizi. Guillemette na Levesque (2006), wanaunga mkono mawazo ya Rimmon-Kenan kuwa umarudio wa tukio hujumuishwa katika vipengele hivyo vitatu vikuu vya wakati simulizi.

Wamitila (2005), anaeleza dhana hii hutumiwa kurejelea mara ambazo matukio hutokea katika hadithi na mara ngapi matukio hayo yanasimuliwa. Mawazo yake vile vile yanakubaliana na ya Rimmon-Kenan na Guillemette.

3.3.1 Umarudio Mara Moja

Rimmon-Kenan (2002), anaeleza kuwa umarudio mara moja ni unenaji mara moja wa tukio lililotendeka mara moja. Huu ndio umarudio unaotumika sana katika usimulizi. Tukio lililotokea mara moja linaweza kusimuliwa mara moja Wamitila (2005). Umarudio mara moja umeakisiwa katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

Vita kati ya Mikidadi na Afriti aliyekuwa akiishi karibu na chemi-chemi ya maji safi vinatokea mara moja tu na tukio hili linasimuliwa mara moja tu. Haya yanaashiriwa katika beti zifuatazo, 175-184.

Mtumwa wake huyule

Akamuata papale

Akenenda polepole

Mai kayafikiria (ubeti 175)

Hata akisa kusoma

Yule jini kalala

Akamba moto wachoma

Muwili wangu jamia (ubeti 181).

Kisa cha mauaji ya Luhani kimesimuliwa mara moja na kimetukia mara moja. Luhani na jeshi lake walikuwa wamemteka nyara Kesi na mkewe Anasa na haja ilikuwa kumuua Kesi ili mkewe Anasa aolewe na mmoja wa wanajeshi. Mikidadi aliwafumania na

kutumia hila kuweza kumfungua Kesi na mkewe na baadaye kumuua Luhani kwa kumkata kichwa. Haya ni katika ubeti 236-238

Akamtaka na rasu

Kwa mkonowe na kisu

Akamwelekea kisu

Mbeleye kamuekea (ubeti 238)

Kisa cha Sultani wa Kisira aliwatuma wanaume mia tano kupigana na Mikidadi na sharti lilikuwa wamkate kichwa Mikidadi na kumpelekea Sultani lakini wengi waliuawa na wengine kutoroka (ubeti 289-300).

3.3.2 Umarudio Mara Nyingi

Rimmon-Kenan (2002), anaeleza kuwa ni usemaji wa tukio moja mara nyingi yaani tukio lililotokea mara moja linaweza kusimuliwa mara kadha.

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* umarudio mara nyingi umetumika ingawa si kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, Mikidadi anarudia mara kadha kuwa atahakikisha atatafuta mahari aliyoitishwa na Jabiri. Anamhakikishia mjombake Turadi, watu na Jabiri mwenyewe kuwa angepata mali hayo yote hata zaidi. Tazama beti 150, 157, 161, 162 na 163.

Akajibu Mikidadi

Ewe mjomba Turadi

Mahari haya budi

Yote yatatimilia (ubeti 157).

Niushikapo upanga
Dunia yote hitangi
Mali yote tayatunga
Haibudi kutimia (ubeti 160).

Msimulizi anarudia tukio hili la kutafuta na kutimiza kiwango cha mahari cha kumposa Mayasa. Aidha mfano mwingine wa umarudio mara nyingi ni kukutana kwa Hamza na Mikidadi, na Hamza akamsaidia kwa mali nyingi na akahakikisha kuwa Mikidadi amesilimu (ubeti 253, 625).

Kitendo cha kunyang'anya watu mali kimerudiwa rudiwa katika masimulizi. Mikidadi aliwavamia watu, majeshi na Sultani kwa kusudi moja tu, kujipatia mahari ya kutosha kwenda kumposa Mayasa.

3.3.3 Umarudio Sisitizi

Rimmon-Kenan (2002), anaeleza ni usimulizi mara moja wa tukio lililotokea mara nyingi katika hadithi, yaani tukio lililotokea mara kadha, linasemwa mara moja.

Guillemette na Levesque (2006), nao wanasema kuwa katika usimulizi tunaweza kuwa na usimulizi wa tukio mara nyingi lililotokea mara nyingi katika hadithi.

Vita kati ya Mayasa na waposi wake vimetajwa tu katika hadithi na walikuwa wengi mno. Msimulizi ameelezea kwa kirefu vita kati ya Mayasa na Mikidadi (ubeti 91-107)

japo hapo awali Mayasa alikuwa amepigana na waposi wengi na baadhi yao waliuawa na wengine kutoroka kwa kuhofia maisha yao.

Tukio kunenwa mara nyingi na kutokea mara nyingi ni arki ambayo ipo katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Mikidadi anaitwa Simba mara nyingi na matokeo ya kijasiri yanayomsawiri simba yanatokea kwingi. Kwa mfano anapopigana na afriti, Luhani na Sultani, washenga wa Maliki na Ali katika kupigania taji la Fatuma. Matendo haya yote ya kijasiri yanathibitishwa katika beti hizi: (ubeti 171-181, 214-220).

3.4 Hitimisho

Katika sura hii tumechunguza mpangilio wa matukio katika hadithi ya *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Mpangilio wa matukio unafuata mikondo mitatu; mpangilio wa matukio katika mfuatano wa wakati, muda katika usimulizi na idadimarudio ya matukio. Hali kadhalika mikondo hii imegawika katika namna mbalimbali za mpangilio wa matukio hayo kama vile, analepsia, prolepsia, masafa na mwanda.

Mpangilio wa matukio kufuatia muda katika usimulizi umegawika katika muhtasari, udondoshi, onyesho na mtuo. Aidha matukio yamepangwa kufuatia umarudio mara moja, umarudio mara nyingi na umarudio sisitizi. Baadhi ya mikondo hii kuna mpangilio wa matukio kufuatia mfuatano wa wakati kianalepsia ndio umetumika kwa kiasi kikubwa ukifuatiwa na matumizi ya onyesho la mawazo.

SURA YA NNE

MTAZAMO

4.0 Utangulizi

Katika sura hii tutachunguza mtazamo katika usimulizi. Wamitila (2008: 140) anaeleza:

“Mtazamo huelezea jinsi tunavyotazama matukio au wahusika katika hadithi inayohusika. Ingawa dhana hii inaelekea kuisisitiza kuwa, ‘mwono’ au ‘mtazamo’ unaozungumziwa unaweza kuhusisha sifa au vipengee vya kisaikolojia na vya kiitikadi”.

Naye Manfred (2005) anaeleza mtazamo kama uchunguzi na ubanaji wa ujumbe wa usimulizi wa kuona matukio na hali ya mambo yaani mwono wa mtu.

Aidha, Rimmon–Kenan (2002) anaeleza kuwa hadithi huwasilishwa katika matini kupitia viingiliaji kati kupitia mwono unaosimuliwa na msimulizi ambao ni lazima uwe wake. Wahakiki hawa wanakubaliana mtazamo ni jinsi tunavyoona matukio katika hadithi. Msimulizi huteua ujumbe wasomaji wanaosoma na mtazamo si lazima uwe wa msimulizi.

Ni kutokana na uhalisi ndiposa kuchunguza mitazamo si kazi rahisi. Hata hivyo, tutafuata ruwaza ya Rimmon - Kenan (2002).

4.1 Mtazamo katika Usimulizi

Mhakiki Rimmon-Kenan (2002) amechunguza swala hili akitumia vipengele viwili; Kigezo cha mahali kulingana na hadithi na kigezo cha udumishwaji. Mtazamo kulingana na mahali unaleta mtazamo ndani na mtazamo nje. Mtazamo nje una ukuruba zaidi na ajenti wa usimulizi. Kwa upande mwingine, mtazamo ndani umo katika matukio yanayosimuliwa. Mtazamo ndani huchukua mkondo wa mtazamo wa mhusika katika hadithi inayosimuliwa na ule wa nje ni mtazamo wa msimulizi ambaye hahusiki katika hadithi.

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* mtazamo nje umebainika. Msimulizi ndiye wakala anayetuwasilishia hadithi na wahusika hawatokei kutusimulia hadithi. Uhalisi huu unadhihirika mwanzoni, kati na mwishoni mwa hadithi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Katika mwanzo wa hadithi, tunasimuliwa kuwa katika ubeti 13 ni kweli Mikidadi hakurithishwa chochote. Katika ubeti wa 484 na 777 ni ithibati kwamba msimulizi anawasilisha hadithi kama wakala. Anatumia juu ya babake Mikidadi na juu ya kisa chenyewe cha Mikidadi na Mayasa.

Suwedi ali tajiri

Ali na mali kathiri,

Ali mwingi wa safari

Mali akajitumia (ubeti 13)

Mwate usimtinde,
Na kumpenda mpende,
Ukituma enede,
Ni kombo namwombea (ubeti 484)

Kisa utendi wa vita
Simulia yalopita
Hijazi yenye matata
Jamaa nimewambia (ubeti 777)

Katika sehemu hizi zote zimeonyesha kuwa, msimulizi ndiye ajenti pekee anayesimulia hadithi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* katika kigezo cha mahali kulingana na hadithi na hivyo kuibua sawia au sura mbalimbali za mitamo ambazo tutaandalia hapa.

4.1.1 Sura za Mtazamo

Sura tatu za mtazamo zimechunguzwa na Rimmon-Kenan (2002), sura ya mwanda wakati na mwanda mahali, saikolojia na itikadi.

4.1.1.1 Sura ya Mwanda Mahali na Wakati

Kwa kurejelea mwanda mahali, Rimmon-Kenan (2002), ameeleza mtazamo nje unachukua mtazamo mithili ya ndege aliye mtini akitazama chini. Kwa hivyo, anaweza kuona matukio kutoka kila upande.

Msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* anauakisi mtazamo huu. Anafahamu hali ya zamani ya Mikidadi pamoja na Mayasa hadi waliposilimu na kuwa waislamu.

Aidha, mwanda mahali, unazua mtazamaji asiyeona kila mahali. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kama tulivyoeleza hapo mbeleni, ni mtazamo wa mfano wa ndege mtini. Kwa kurejelea mwanda wakati, mtazamo nje unazua mtazamo wa msimulizi anayejua habari zote za hadithi. Ilhali mtazamo ndani ni mtazamaji asiyejua mengi isipokuwa tu yale anayosimuliwa. Kwa kurejelea mwanda wakati, msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* anatazama hadithi kutoka nje. Kwa hivyo ana ujuzi wa mambo yote ya kabla, sasa na wakati ujao kihadithi. Mathalani: anafahamu umasikini wa Mikidadi, uchungaji mifugo wa Mikidadi, kukataa kwa Mayasa kuolewa na tajiri bali shujaa wa vita, pigano la Mikidadi na Mayasa na ushindi wa Mikidadi ndiposa Mayasa akamteuwa amwoe, mahari aliyoitishwa na mjomba wake ili amwoe Mayasa, mbinu za Mikidadi kukusanya mahari, ujanja wa mjomba wa Mikidadi kumwoza Maliki Mayasa, kurejea kwa Mikidadi na kumwoa Mayasa, jaribio lingine la mjomba wa Mikidadi kumwoza Mayasa na kutekwa nyara kwa Mikidadi na Waislamu kumkomboa Mikidadi kabla ya kuuawa na Jabiri kwa kuwa alikuwa amekwisha silimu.

4.1.1.2 Sura ya Saikolojia

Sura ya saikolojia inahusu mawazo na hisia. Sura ya mawazo inahusu usimulizi wa msimulizi anayejua yote na usimulizi wa msimulizi anayejua machache, kimawazo. Mtazamo nje unaakisi msimulizi anayejua mambo mengi na mtazamo ndani unaakisi

msimulizi asiyejua mengi kuhusu hadithi. Hii inashabihiana na mwanda wakati, kwani msimulizi husimulia yaliyo katika mawazo yake.

Kwa kurejelea sura ya saikolojia hisia, mtazamo nje huzua mtazamo horomo na mtazamo ndani huwa wa kujihusisha. Msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, amedumisha uhoromo katika maelezo yake bila kuingiza hisia zake kali kuhusu yanayohadithiwa.

4.1.1.3 Sura ya Itikadi

Itikadi ni jumla ya kutazama ulimwengu kidhana. Itikadi kuu ni ile ya msimulizi. Kama kuna itikadi nyingine huwa ndogo na huwa zinaelezwa kupitia wahusika. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* mtazamo mkuu ni wa msimulizi. Itikadi yake inafungamana na dini hivyo, kuwa ndiyo itikadi kuu. Arki hii imedhihirika mara tu msimulizi anaanza kusimulia kwa kudokeza hali ya unyenyekevu, heshima kwa Mungu na imani yake kwa Mungu. Hali kadhalika anataja vita vya jihad ambavyo tunaelewa kulingana na Waislamu ni vita takatifu. Aidha, anasimulia juu ya siku ya kiama na ndivyo tunaona Mikidadi na Mayasa wakisilimu na kumwamini Mtume Mohammed kama Mtume pekee wa Mungu angalau wafike paradiso baada ya kifo.

Ubeti wa 1 na 2 unadhihirisha itikadi ya kidini ya msimulizi.

Bismillahi mbuyaza

Awali ya kujifunza

sijui taufawaza

Au vitanichachia (ubeti 1)

Kwa kuwa sina makini

Sina fahamu moyoni

Kwa dunia kuwa duni

Tangu sasa nawambia (ubeti 2)

4.2 Hitimisho

Katika sura hii tumechunguza mtazamo. Mtazamo umegawika katika mtazamo nje na ndani. Mtazamo huu unazua sura mbali mbali kama mwanda mahali na wakati, saikolojia na itikadi. Kila mojawapo wa mtazamo mkuu unazua sura hizi. Mathalani sura ya mwanda wakati, unazua katika mtazamo nje msimulizi anayejua mengi kiwakati au machache. Msimulizi wa *Utendi wa Makidadi Mayasa* ni msimulizi anayejua mengi kiwakati. Kwa kuzingatia mahali, msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi wa Mayasa* ni msimulizi aliye mfano wa ndege aliye mtini akiangalia chini. Sura ya saikolojia katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* inadhihirisha msimulizi mjua yote kimawazo na msimulizi horomo kihisia. Hatimaye, kiitikadi, *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, una itikadi moja kuu tu, ambayo ni ya kidini inayosimuliwa na msimulizi.

SURA YA TANO

UWASILISHAJI WA USEMI NA MAWAZO

5.0 Utangulizi

Wananaratolojia aidha wanajishughulisha na uwasilishaji wa usemi na mawazo. Wamitila (2008), ameshughulikia swala hili vizuri kuliko alivyofanya Rimmon–Kenan (2002). Kwa hivyo katika sura hii, tutajadili kipengele cha uwasilishaji wa usemi na mawazo, tukirejelea Wamitila (2008).

Wamitila (2008) ametofautisha kati ya uwasilishaji wa usemi na mawazo kidaigesia na kimimesia. Ameeleza;

“Usemi unaopatikana katika kazi ya kifasihi unaweza kuwasilishwa kwa njia kadha. Njia kuu ni maelezo ya msimulizi. Hii ndiyo ambayo inaelezwa na wananadharia wa kinaratolojia kama daigesia. Kinyume chake ni pale ambapo lugha ya wahusika inawakilishwa kwa njia iliyo wazi. Wahusika wanajibizana katika mazungumzo na kwa njia hii kuakisi hali halisi kama ilivyo katika drama. Hali hii hujulikana kama muhakati au mimesia”.

Licha ya kuwa hali hizo mbili zinaweza kuonekana kuwa tofauti, hali hizo mbili zinachangiana na hata kusaidiana.

Wamitila (2008) ameorodhesha mikakati minane ya kuwasilisha usemi na mawazo. Mikakati hii ni usemi halisi, mawazo halisi, usemi taarifa, mawazo taarifa, usemi halisi huru, mawazo halisi huru, usemi taarifa huru na mawazo taarifa huru.

5.1 Usemi Halisi na Mawazo Halisi

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), usemi halisi ni uwasilishaji wa maneno yatamkwayo na msemaji (mhusika) kama alivyoyasema kwa kutumia alama za unukuzi. Hali mawazo halisi pale ambapo kinachowasilishwa si maneno bali mawazo ya mhusika yanavyompitikia akilini.

Utendi wa Mikidadi na Mayasa hauonyeshi uwasilishaji wa usemi halisi na mawazo halisi. Kwa hivyo hatuna mifano ya uwasilishaji wa mawazo na usemi huu kutoka utenzini.

5.2 Usemi Halisi Huru na Mawazo Halisi Huru

Wamitila (2008), ameeleza kuwa usemi halisi huru hutokea pale ambapo vishikizi vya kauli ya msemaji na alama za nukuu za kuonyesha kuwa huo ni usemi halisi zinaondolewa. Licha ya ondoleo hilo la nukuzi, maneno hubakia tu kama kwenye usemi halisi. Ikiwa kinachowasilishwa ni mawazo basi uwasilishi huwa uwasilishi wa mawazo halisi huru.

Utendi wa Mikidadi na Mayasa unaakisi mtindo huu wa kuwasilisha usemi na mawazo.

Kwa mfano ubeti 24, tunasimuliwa;

Wakenda masultani,

Na mali yao ndiani

Akanena Sufyani

Sina budi tamuoa

Maneno ya Sufyani yanaweza kuwasilishwa kama:

Akanena Sufyani, “Sina budi tamuoa”.

Kukosekana kwa vishikizi vya usemi halisi vinabadilisha mtindo wa kupelekea kuwa uwasilishaji wa usemi na mawazo halisi huru.

Aidha, ubeti 28, unaakisi sifa hii ya usemi halisi huru na kwa vile mishororo mitatu ya mwisho yanaweza kuwa usemi halisi maadamu tu itiliwe alama za unukuzi kama ifuatavyo :

Waposi wakamwambia, ‘Tujile tuna shauri, tuna mali akthari kwa kutaka ndoa’

Wakamwambia Jabiri

Tujile tuna shauri

Tuna mali akthari

Tujile kutaka ndoa

Beti nyingine zenye kuakisi uwasilishaji huu ni: 29, 30, 31-32, 37-40, 51-54, 67-74, miongoni mwa nyingine.

Licha ya mifano hii ya uwasilishaji wa usemi, *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* hauonyeshi uwasilishaji wa mawazo.

Matumizi ya usemi halisi huru, kwa mujibu wa Wamitila (2008) una dhima mbili kuu:

mara nyingine huweza kuingiza hisia na mtazamo wa msimulizi, na unafungamanisha sauti ya msemaji na usimulizi na kuzifanya kuwa kama sauti moja. Hizi dhima hufanya usimulizi kuakisi zaidi daigesia.

5.3 Usemi Taarifa na Mawazo Taarifa

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), usemi taarifa na mawazo taarifa, unahusisha uwasilishaji maneno kama ripoti ya yaliyotamkwa au kumpitikia mhusika akilini. Hata hivyo usemi taarifa unatambulika kwa kutotumika kwa alama za unukuzi. Pili, huwa na maneno kama “kwamba”. Tatu, viwakilishi vya nafsi ya kwanza na pili hubadilika na kuwa nafsi ya tatu. Nne, viashiria vya mahali na wakati hubadilika. Hatimaye vitenzi hubadilika kutoka mwelekeo wa “kuelekea” hadi “mbali na”.

Utendi wa Mikidadi na Mayasa, unaakisi mtindo huu wa uwasilishaji katika beti za 13 na 14 mtawalia :

Suwedi ali tajiri

Ali na mali kathiri

Ali mwingi wa safari

Mali akajitumia

Hata alipotoweka

Mali yakatawanyika

Asipate cha kushika

Yote yakampotea

Beti hizi mbili zinaakisi nafsi ya tatu. Hivyo, ni uwasilishaji wa usemi taarifa. Hali kadhalika, uwasilishaji mawazo katika mtindo wa taarifa unajitokeza katika ubeti 101:

Mikidadi juhudiye

Ataka amwangelie

Na Mayasa bidiyie

Hataki kumtambua

Maelezo katika ubeti huu yanaashiria kitendo cha kutaka, ambacho si cha kutendeka bali kinachowapitikia Mikidadi kwa upande mmoja na Mayasa kwa upande mwingine akilini mwao. Kwa hivyo ni tamaa ya wawili hawa ndio inawasilishwa. Hivyo kufaulu kuwa uwasilishaji wa mawazo.

Hali kadhalika ubeti 508, unaakisi mtindo huu wa kuwasilisha usemi taarifa na mawazo taarifa :

Na Mayasa hamtaki

Kuolewa na Maliki

Bin Riyahi Atiki

Lakini wajifanyia

Swala la Mayasa kukataa ndoa ya Maliki ni la mawazo wala is la kuonekana kutoka nje.

5.4 Usemi Taarifa Huru na Mawazo Huru

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), usemi taarifa ukifanyiwa mabadiliko kwa kuondoa maneno yanayoashiria taarifa, pengine na kuacha sifa zinazohusishwa na usemi halisi, matokeo yake ni usemi taarifa huru. Vivyo hivyo, kama kiwasiliwacho ni mawazo ya kuhusika, matokeo yake ni mawazo huru.

Mtindo huu wa uwasilishaji wa usemi, unahusika katika fomula ya ufunguzi na fomula ya kutamatisha utenzi. Fomula ya ufunguzi katika ubeti 1 hadi 11, hali kadhalika fomula tamatishi katika ubeti 778.

Nami mwenye kuradidi,

Isimu yangu Saidi

wa Abdalla Masudi

Jina langu nawambia

Licha ya kuwepo kwa usemi taarifa huru, *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* hauonyeshi uwasilishi wa mawazo huru.

5.5 Hitimisho

Katika sura hii tulichunguza uwasilishaji usemi na mawazo. Uwasilishaji unaweza kuwa wa kidaigesia au kimemisia. *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unatumia uwasilishaji wa kidaigesia. Hali kadhalika tulipata kuwa uwasilishaji wa usemi na mawazo halisi haukupatikana katika *Utendi wa Mikidadi ya Mayasa*.

Uwasilishaji wa usemi halisi na mawazo halisi hunena mawazo huru, ulidhihirika tu katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* katika usemi tu, mawazo hayakupatikana.

Uwasilishaji wa usemi taarifa na mawazo taarifa ulipatikana katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Hatimaye, uwasilishaji wa usemi taarifa huru na mawazo taarifa huru, unajitokeza tu katika kipengele cha usemi lakini mawazo hayawasilishwi kitaarifa huru katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

SURA YA SITA

HITIMISHO

6.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tunashughulikia matokeo ya utafiti wetu na mikakati tuliyotumia ili kufikia madhumuni yetu. Tulikusudia kuchunguza iwapo sifa za simulizi bunilizi zinazohusishwa katika riwaya zinaweza kupatikana katika ushairi wa kale wa Kiswahili. Sifa tulizozitalii ni pamoja na usimulizi, mpangilio wa matukio katika hadithi, mtazamo na uwasilishaji wa usemi na mawazo katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

6.1 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti wetu umejikita katika uhakiki wa arki za simulizi bunilizi katika *Utendi wa kale wa Kiswahili wa Mikidadi na Mayasa*. Ni utendi uliotungwa na Said Abdallah Masudi el Buhry miaka mingi kabla ya karne ya ishirini na ni baadhi ya tungo zilizo ndefu sana. Utendi huu umehakikiwa na Mungai P. K. (2005), katika ulinganishi wa kifani na *Utendi wa Swifa ya Nguvumali*. Tumechagua kuendeleza kazi hii ya Mungai kwa kuhakiki utendi huo tukitumia nadharia ya naratorojia mwelekeo wa Rimmon-Kenan (2002).

Tumechunguza arki zinazopatikana na jinsi zinavyotumika kujenga *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Ni dhahiri kwamba jumla ya arki ambazo tumezichunguza angalau asilimia tisaini zimetumika na kuchangia pakubwa katika uwasilishaji wake.

Katika sura ya kwanza ni utangulizi ambapo tumeanza kwa kundokeza muhtasari wa kisa cha *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Tumetambua ya kwamba ni utenzi wa kale na unao itikadi za kiislamu. Tumbainisha somo letu la utafiti baada ya kusoma kwingi na kugundua kuwa utafiti wa ushairi wa kale umefanywa na wengi lakini wachache mno ambao wamejikita katika uhakiki wa kinaratolojia wa tendi. Kwa hivyo, tumefanikiwa kuendeleza tafiti za simulizi bunilizi kama kiunzi kimoja cha kipengee cha kinaratolojia katika mashairi ya kale.

Katika kushughulikia upeo na mipaka tumejikita katika matini yenyewe ya kisa cha Mikidadi na Mayasa, nadharia ya naratolojia hasa mwelekeo wa Rimmon-Kenan (2002) na uchunguzi wa sifa za simulizi bunilizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Baada ya kusoma hayo yote tumbainisha arki za simulizi bunilizi katika utendi.

Tumeelezea kwa kina msingi wa nadharia ya naratolojia na yaliyoandikwa kuhusu somo hili. Wananaratolojia hawa wametuwekea msingi wa kujadili mada yetu. Wasomi nao ambao wamefanya tafiti za ushairi wa kale, kazi zao zimetusaidia kwa marejeleo na mwongozo wa kazi yetu.

Kimsingi, mbinu za utafiti huu umekuwa wa maktabani ambapo tumesoma tenzi mbalimbali za kale, tasnifu zinazohusu ushairi, vitabu, majarida na machapisho. Mtandao umekuwa nguzo muhimu katika utafiti wetu. Utafiti ambao tumeufanya tumepata arki za simulizi bunilizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kama ilivyoelezewa hapa chini kulingana na kila sura.

Katika sura ya pili tumehakiki usimulizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Katika kipengele hiki cha usimulizi, usimulizi nje unajitokeza zaidi kama inavyothibitishwa na beti nyingi kuanzia 12 hadi ubeti wa 776. Hata hivyo ruwaza hii inakiukwa na fomula ya ufunguzi na fomula ya kufunga, msimulizi anapojihusisha katika hadithi. Beti 1-12 anaomba Mola na kumshukuru kwa kumpa maarifa ya kutunga utendi huu wa Mikidadi na Mayasa. Aidha, katika kuhitimisha hadithi, msimulizi anajitambulisha kwa majina hivyo kuhusika katika hadithi. Kwa hivyo *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaonyesha msimulizi mseto yaani msimulizi ndani na nje umejitokeza.

Katika viwango vya usimulizi imedhihirika kwamba kiwango cha hadithi kuu ndicho kinachotawala katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Usimulizi wa kisa hiki basi ni wa daraja ya kwanza kwa kuwa hadithi yenyewe haijaegemezwa vijihadithi vingine bali vijihadithi vilivyoko ndivyo vimeegezwa kwenye hadithi kuu.

Kwa upande mwingine tumechunguza mhusika licha ya kupuuzwa kwa kipengele hiki na wahakiki wa kisasa, tumechunguza kupitia mtazamo wa wanaratolojia wakongwe (kirasimu) wa Greimas na Ewen. Jambo ambalo limetufanya kugundua kuwa ni eneo linalohitaji kufanyiwa uchunguzi na utafiti wa dhati kama vile walivyofanyia vipengele vingine.

Rimmon- Kenan (2002), ameeleza kuwa, arki yoyote katika matini inaweza kuakisi uhusika. Hii ina maana kuwa, uhusika unaweza kudavuliwa kupitia arki nyingi katika

matini. Kuna viakisi viwili vya uhusika katika matini. Viakisi vinaweza kuwa dhahiri au visiwe dhahiri na vimethibishwa katika maelezo yetu.

Katika kipengele cha wakati wa usimulizi tumethibitisha kwamba usimulizi baadaye ndio unaotamalaki usimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Msimulizi anasimulia kilichotendeka wakati uliopita wakati huu kihadithi. Matumizi ya viambishi 'lo' yaani 'li' na 'me' itatafsiriwa kama hadithi yenyewe ni ya zama japo usimulizi wenyewe umekamilika hivi punde. Usimulizi kabla umejitokeza nadra sana katika matukio mawili yanayohusu kusilimu kwa Mikidadi na Mayasa kwa sababu ya siku ya kiamama. Usimulizi sambamba unapatikani kwa kiasi kidogo sana wakati msimulizi anpoitisha kitabu aanze kutunga shairi katika utangulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

Utendi wa Mikidadi na Mayasa unadhihirisha msimulizi mtegemefu kulingana na vigezo vya Rimmon-Kenan (2002) vya msimulizi kuwa ameonyesha ujuzi wa kutosha kuhusu hadithi yake japo inapatikana kitabuni. Msimulizi anaelewa yote yanayotendeka katika hadithi ingawa hakushiriki katika hadithi yenyewe.

Kulingana na hadhi ya msimulizi, usimulizi wa kidaigesia umedhihirika zaidi kuliko ilivyo kimimesia. Msimulizi amechagua mbinu ya kuhadithia bila kuhusisha kuonyesha vitendo. Katika kutathmini uhusika na mhusika ni wazi kwamba sifa hii ya kisimulizi inapatikana katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

Katika sura ya tatu, tumebainisha sifa za mpangilio wa matukio katika mfuatano wa wakati. Ingawa baadhi ya arki katika kipengele hiki zimetumika kuliko zingine. Analepsia imetamalaki utendi kuliko ilivyo prolepsia. Hali kadhalika muhtasari umetumika kuliko ilivyo onyesho, mtuo na udondoshi. Kipengele cha idadimarudio kimebainika katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

Kulingana na kipengele cha mtazamo katika usimulizi, sura zote za mtazamo, itikadi, saikolojia na mwanda mahali na mwanda wakati zimejitokeza katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Msimulizi adhihirisha kujua mengi kiwakati, kimawazo na msimulizi horomo kihisia. Hali kadhalika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* una itikadi moja kuu tu ya kidini inayosimuliwa na msimulizi.

Katika sura ya tano tumechunguza uwasilishaji wa usemi na mawazo. Uwasilishaji wa usemi halisi huru na mawazo halisi huru ulijitokeza katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* katika usemi tu, mawazo hayakupatikana. Uwasilishaji wa usemi taarifa na mawazo taarifa ulipatikana katika utendi. Hata hivyo tulipata kuwa uwasilishaji wa usemi halisi na mawazo halisi haukupatikana katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Aidha, uwasilishaji wa usemi taarifa huru na mawazo taarifa huru unajitokeza tu katika kipengele cha usemi lakini mawazo hayawasilishwi kitaarifa huru katika utendi huu.

Kulingana na uchunguzi huu ni dhahiri kwamba elementi nyingi za usimulizi zinapatikana katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Kwa hivyo, arki za simulizi bunilizi zinazohusishwa na riwaya zinaweza kupatikana katika tendi za kale za Kiswahili.

6.2 Mapendekezo

Nadharia ya naratolojia ni pana sana hivyo yale ambayo tumeyashughulikia ni machache mno. Kuna mwanya mkubwa sana wa kuhakiki tenzi za kale kwa kutumia mikabala mingine ya kinaratolojia.

Kuna haja ya wahakiki wa baadaye kuchunguza arki za simulizi bunilizi ambazo hatukutafiti kama vile jukumu la kuhadithia, jukumu la uelekezaji, jukumu la mawasiliano, jukumu la kiitikadi na jukumu la ushuhuda katika kipengee cha kuonekana kwa msimulizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Ni muhimu pia kuchunguza sauti katika usimulizi, hali katika usimulizi na mahasa katika usimulizi ili kuelewa zaidi *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kwa vile utafiti wetu umejikita tu katika baadhi ya vijenzi vya kimuundo vya usimulizi.

Tumechunguza mhusika licha ya kupuuzwa kwa kipengee hiki na wahakiki wa kisasa. Tumehakiki kupitia mtazamo wa wananaratolojia wakongwe (kirasimu) wa Greimas na Ewen. Jambo ambalo limetufanya kugundua kuwa ni eneo linalohitaji kufanyiwa uchunguzi na utafiti wa dhati kama vile walivyofanyia vipengee vingine kwa sababu lina utata. Kuchunguza uhusika na mhusika katika miktadha tofauti ya hadithi na matini ndio yanayozidisha utata huu. Ingalikuwa bora kama dhana hizi zingejumuishwa katika muktadha mmoja.

Rimmon-Kenan (2002), anaeleza kuwa naratolojia bado ina uamilifu muhimu katika ulimwengu wa sasa, lakini inapaswa kuboreshwa na kuhusishwa na mielekeo mingine ya kihakiki. Kwa sasa nadharia hii ina matawi kama naratolojia ya ufeministi, umaksi, asilia ya baada ya ukoloni, ya baada ya usasa, ya mawazo na ya muktadha. Tunaunga mkono mapendekezo ya Rimmon-Kenan kuwa tenzi za kale zinaweza kuhakikiwa kutumia mikabala hiyo kama inavyotumiwa katika kuhakiki riwaya.

6.3 Hitimisho

Madhumuni yetu yalikuwa kuchunguza ikiwa arki za simulizi bunilizi zinapatikana katika utendi wa kale wa Kiswahili wa *Mikidadi na Mayasa* katika uwasilishaji wake. Lengo lingine la utafiti wetu lilikuwa tuonyeshe ya kwamba arki za kisimulizi zimetumika kujenga *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kama ilivyo katika riwaya. Ni kweli *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaakisi sifa za kisimulizi. Tumethibitisha kwamba arki hizi zinapatikana katika utendi na zimetumika kujenga *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Msimulizi amefanikiwa kuwasilisha utendi huu kama usimulizi.

MAREJELEO

- Allen, J. (1971): *Tendi*. Nairobi: Heinemann.
-
- (1991): *A Poem Concerning the Death of Prophet Mohammed*. New York: E Mellen Press.
- Barthes, R. (1970): *An Introduction to the Structural Analysis of Narrative: New Literary History*. New York: Cambridge University Press.
- Dammann, P. (1940): *In Dichtugen der Lamu Mundert des Suaheli*. Hamburg Feiderichen: De Gruyeter & Co.
- Davis, C. na Schleifer, R. (1989): *Contemporary Literary Criticism: Literary and Cultural Studies*. 2nd Edition, New York and London: Longman.
- Fokkema, D. (1997): *Theories of Literature in the Twentieth Century*. London: C. Hurst and Company.
- Forster, E. (1927): *Aspects of the Novel*. London: Penguin Books.
- Genette, G. (1972): *Narrative Discourse*. Trans. Jane E. Lewin. Oxford: Blackwell.
- Greimas, A. (1966): *Semiotic Structures katika Seldan*. New York: Cambridge University Press.
[Online].

- Guillemette, L. na Levesque, C. (2006): *Introductory Guide to Critical Theory*: in Dino, F. 'Modules on Barthes; On Plotting [Online].
- Harries, L. (1962): *Swahili Poetry*. Oxford: The Claredon.
- Hichens, W. (1972): *al-Inkishafi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kezilabahi, E. (1997): "Creative Writing in Swahili" Makala ya Kongamano la Uandishi wa Kibunifu Katika Lugha za Kiafrika. SOAS, London.
- Knappert, J. (1964): *Four Swahili Epics*. Leiden: Drukkerij, Luctor et Emergo.
-
- (1967): *Traditional Swahili Poetry: An Investigation into the Concept of East African Islam as Reflected in the Utenzi Literature*. Leiden: E.J. Brill.
-
- (1979): *Four Centuries of Swahili Verse*: Leiden: E J. Brill.
- Lambert, E. (1965): *Ode to Mwana Mnga*: Bulletin No. 23 in the East African Inter-Territorial Language Committee.
- Manfred, J. (2005): *Narratology: A Guide to the Theory of Narrative*. English Department, University of Cologne.

- Mbatiah, M. (2001): *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbook & Graphics and Publishing.
- Mungai, P. (2005): “*Uhakiki linganishi wa kifani wa Tenzi Mikidadi na Mayasa na Swifa ya Nguvumali*”, Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha. Nairobi. (Haijachapishwa).
- Murage, J. (2011): *Uhakiki wa Fani katika Utendi wa Mwana Ninga*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Mutiso, W. K. (1985): “*Hurafa na Uyakinfu katika Hamziyyah*”. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
-
- (1996): “*Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida ya Burudai*”. Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
-
- (2003): *Analysis of Swahili Islamic Poetry: Five Swahili Epic by Four Swahili Women*. (Haijachapishwa).
-
- (2005): *Utenzi wa Hamziyyah*. Institute of Kiswahili Research, University of Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam.
- Rimmon-Kenan, S. (2002): *Narrative Fiction*. London: Routledge.

- Olali, T. (2004): *The Veneration of the Prophet: The Role of Hamziyyah During the Maulidi Festival of the Lamu, Archipelago, Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo kikuu cha London.
- Seldan, R. (1995): *The Cambridge History of Literary Criticism: From Formalism to Post structuralism*, Volume 8. New York: Cambridge University Press.
- Shitemi, M. (2011): *Usimulizi katika Utenzi wa Siri li Asirali*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.
- TUKI, (2006): *English-Kiswahili Dictionary: 3rd Edition*. Dar es Salaam.
- Wamitila, K. (2003): *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi : Phoenix Publishers.
- _____ (2005): *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na vipengee vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- _____ (2006): *Uhakiki wa Fasihi Nadharia na Misingi yake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- _____ (2008): *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa & Publishers Ltd.

Werner, A.

(1932): *Hadithi ya Miqdad na Mayasa*. Medstead
Hempshire: The Azania Press. 81.